# Nipashe

Ijumaa Juni 14, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579944

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mwanamke jela miezi sita kujaribu kumuua mwanawe

UKURASA 12


UCHUMI

Huawei imeegeshwa hatarini kupoteza hadhi ya'simu janja'

ILO: Hawa ndio watumishi wa ndani wanaishi hivi

BUFE

Ijumaa Juni 14, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Hoja sita 'zilizoshindikana' Bunge la Bajeti

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# BAJETI YA 2019/20 YABANA, YAPULIZA




HABARI UKURASA 2 & 3

## TAMU

- Kicheko watumiaji wa bia na sigara
- Tozo 54 TFDA, TBS, Mkemia Mkuu zafutwa
- Ushuru asilimia 0 malighafi nepi za watoto
- Msamaha makasha ya kuhifadhia mboga
- Msamaha kodi tiketi za ndege, kalenda, sare watumishi ndege
- Kufutwa VAT umeme kwenda Zanzibar
- Tozo ukaguzi maduka mapya vyakula
- Hakuna kodi mauzo ghafi chini ya mil. 4/-
- Msamaha ushuru vifaa kukatia madini
- Hakuna VAT makaratasi ya vifungashio
- Ushuru vifungashio vya mbegu 'out'



## MACHUNGU

- Ongezeko asilimia 10 kodi mawigi
- Kodi taulo za kike
- Leseni udereva 70,000/-
- Usajili magari, Bajaji, bodaboda juu
- Ushuru mabomba

# Kada wa Chadema adaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi

UKURASA 4

MICHEZO **SIMBA YAIZIDI UJANJA YANGA** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Akiba fedha za kigeni Dola bil. 4.4/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imelieleza Bunge kuwa akiba ya fedha za kigeni ni Dola za Marekani bilioni 4.395.

Akiwasilisha bungeni jana taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema akiba iliyopo inatosha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.3.

Waziri huyo alisma akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kuendelea kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi na kuongeza imani kwa wawekezaji katika uchumi.

"Akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani milioni 4,395.2 Aprili 2019, kiasi ambacho kinatosha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takribani miezi 4.3," Dk. Mpango alisema.

Aliongeza kuwa kiwango hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi minne.

**THAMANI YA SHILINGI**

Katika taarifa yake hiyo, Dk. Mpango pia alisema thamani ya shilingi imeendelea kuwa imara, akibainisha kuwa katika kipindi kilichoishia Aprili mwaka huu, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh. 2,300.9 ikilinganishwa na Sh. 2,270.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

"Utulivu katika mwenendo wa thamani ya shilingi umetokana na utekelezaji wa Sera ya Fedha, matumizi ya gesi asilia badala ya mafuta katika kuzalisha umeme na baadhi ya viwanda kuzalisha bidhaa ambazo awali zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje vikiwamo vigae na marumaru," alisema.

Dk. Mpango alisema katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni, Novemba mwaka jana, Benki Kuu (BoT) ilifanya ukaguzi wa ghafla katika maduka ya kubadilisha fedha jijini Arusha na kuyafunga maduka yasiyozingatia taratibu na kisheria za biashara hiyo.

Vilevile, alisema Februari mwaka huu, BoT ilifanya ukaguzi wa kawaida wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni jijini Dar es Salaam na kubaini kwamba maduka mengi yanaendesha biashara hiyo pasipo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni.

"Kufuatia ukaguzi huo, BoT ilianza utaratibu wa kufuta leseni za maduka yote yaliyokutwa yanaendesha biashara hiyo bila kuzingatia masharti ya leseni ambapo zoezi hili linaendelea," alisema.

**DENI LA SERIKALI**

Waziri Mpango alibainisha kuwa hadi Aprili mwaka hu, Deni la Serikali lilifikia Sh. trilioni 51.036 ikilinganishwa na Sh. trilioni 49.866 Aprili 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.4.

"Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilifikia Sh. trilioni 13.251 na deni la nje Sh. trilioni 37.785.76. Ongezeko la deni lilitokana na kupokewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa, madaraja ya juu na miradi ya barabara," alisema.

Waziri Mpango alisema tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba mwaka jana ilionyesha nchi ina uwezo wa kukopa ndani na nje na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya fedha.

"Katika kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu, serikali itaendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha mikopo inaelekezwa kwenye miradi ambayo itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi," alisema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, Gavana wa Benki Kuu, Prof. Florens Luoga na watendaji wakuu wa wizara hiyo na taasisi zake wakiwa katika jukwaa la Spika wakifuatilia taarifa ya hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mipango, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

## BAJETI 2019/20

# Yabana, yapuliza

**Augusta Njoji na Sanula Athanas,** DODOMA

NI shangwe na kilio. Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha kuwa na mambo mengi yanayofurahisha na machache kuumiza.

Makadirio hayo ya kukusanya na kutumia Sh. trilioni 33.11, yaliwasilishwa bungeni jijini Dodoma jana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Katika hotuba yake, Dk. Mpango aliibua shangwe bungeni alieleza kuwa anapendekeza kufuta baadhi ya tozo zinazolalamikiwa kuwa kero katika biashara na uwekezaji.

Dk. Mpango mbali na kupendekeza kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika baadhi ya bidhaa, aliibua shangwe alipotangaza kuwa serikali inakusudia kufuta tozo 54 kwa lengo la kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji nchini.

Tozo hizo 54 ni zinazotozwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa uchumi aliibua minong'ono alipoeleza mapendekezo machache ambayo yalionekana kutowafurahisha watunga sheria hao.

Katika mapendekezo yake, Dk. Mpango aliibua shangwe alipoeleza kuwa serikali inakusudia kufuta tozo mbalimbali zikiwamo zilizolalamikiwa na wafanyabiashara waliokutana na Rais John Magufuli Ikulu jijini Dar es Salaam Juni 7, mwaka huu.

Tozo na ada zinazopendekezwa kuongezwa na kuonekana kutowafurahisha wabunge, ni pamoja na ongezeko la ada ya usajili wa magari kutoka Sh. 10,000 hadi Sh. 50,000, ongezeko la ada ya leseni ya udereva kutoka Sh. 40,000 hadi Sh. 70,000, kurejeshwa kwa VAT katika taulo za kike na tozo ya nywele za bandia zinazozalishwa nchini na kuagizwa nje.

**SURA YA BAJETI**

Dk. Mpango alisema kwa kuzingatia shabaha, malengo na Sera za Bajeti kwa Mwaka 2019/20, sura ya bajeti inaonyesha kuwa, jumla ya Sh. trilioni 33.11 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho.

Alibainisha kuwa jumla ya mapato ya ndani yanarajiwa kuwa Sh. trilioni 23.05, sawa na asilimia 69.6 ya bajeti yote.

Waziri huyo alisema kati ya mapato hayo, serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya Sh. trilioni 19.1, sawa na asilimia 12.9 ya Pato la Taifa.

Alisema mapato yasiyo ya kodi kwa mwaka 2019/20 yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 3.18 na mapato kutoka vyanzo vya

INAENDELEA UK.8

# Serikali yarejesha kodi taulo za kike

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema inakusudia kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika taulo za kike iliyoiondoa mwaka jana.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, hotuba kuhusu mapendekezo kuhusu bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema anapendekeza kurejesha kodi hiyo baada ya kubaini uamuzi uliofanyika haujawezesha kupatikana kwa unafuu wa bei kwa walengwa.

Dk. Mpango pia alisema anapendekeza kufuta VAT kwa umeme unaokwenda visiwani Zanzibar.

Katika hotuba yake hiyo, waziri huyo alisema anapendekeza kufuta msamaha wa VAT uliokuwa umetolewa kwenye taulo za kike kwa kuwa haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara.

"Wakati serikali ilipoweka msamaha huu, ilitarajia kwamba wazalishaji wa taulo za kike wataziuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi," alisema.

Waziri huyo pia alisema anapendekeza kufuta kodi kwenye makasha yenye majokofu yanayotumika kwenye kilimo cha kisasa cha mboga kwa wakulima wanaoingiza makasha hayo kutoka nje ya nchi.

Alisema lengo la hatua hiyo ni kupunguza gharama na kutoa unafuu katika uzalishaji na kuhamasisha kilimo cha kisasa cha mboga nchini.

Alisema anapendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 68(3)(d) ili kisihusishe uuzaji wa mazao ghafi ya kilimo nje ya nchi.

"Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wauzaji wa mazao ghafi ya kilimo nje ya nchi kuendelea kufanya biashara hiyo kwa kadri ya kibali kitakavyotolewa na serikali," alisema.

Dk. Mpango alisema VAT pia imesamehewa kwenye vifaa vya kukaushia nafaka.

"Msamaha huu unatarajiwa kutoa unafuu

INAENDELEA UK. 26

## HABARI KITAIFA

# Tozo 54 kufutwa TBS, TFDA

**Sanula Atanas na Romana Mallya**

SERIKALI imependekeza kufuta tozo 54 zinazotozwa na wizara, idara na mamlaka za udhibiti kwa lengo la kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji nchini.

Akiwasilisha bungeni jana mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema hatua hiyo imechukuliwa kutokana na matokeo ya mkutano wa Rais John Magufuli na wafanyabiashara uliofanyika hivi karibuni Ikulu jijini Dar es Salaam.

Dk. Mpango alisema ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa yenye manufaa kwa taifa kama vile ujenzi wa miundombinu, ununuzi wa ndege, mabehewa au vichwa vya treni, serikali pia inapendekeza kurekebisha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015 kwa lengo la kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuongeza muda wa matumizi ya fedha za mwaka wa fedha uliomalizika hususan zinazohusu miradi ya maendeleo.

Alisema sheria hiyo kwa sasa imeweka ukomo wa miezi mitatu wa kutumia fedha za mwaka uliomalizika na baada ya muda huo, fedha hupaswa kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Dk. Mpango alisema kufuatia matokeo ya mkutano wa Rais Magufuli na wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini uliofanyika hivi karibuni, serikali inapendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo 54 zinazotozwa na wizara, idara na taasisi zinazojitegemea ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Alisema hatua hiyo imelenga kuondoa mwingiliano wa majukumu ya kiutendaji baina ya wizara, taasisi na mamlaka za udhibiti.

Katika kutekeleza hatua hiyo, waziri huyo alisema katika Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), anapendekeza kufuta tozo za kushikilia usajili wa dawa za chanjo inayotozwa kwa Dola za Marekani 150, dawa za mitishamba Dola 100, vitendanishi Dola 250 chakula Dola 100, vipukusi Sh. 100,000 na tozo za bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi.

Dk. Mpango alisema pia anapendeza kufuta tozo za kudurufu cheti cha usajili wa vitendanishi inayotozwa kwa kiasi cha Dola 100, tozo ya ukaguzi wa maduka mapya ya kuuzia vyakula Sh. 50,000, tozo ya usajili wa maduka ya rejereja ya dawa za mifugo ambayo ni kati ya Sh. 50,000 na 100,000.

Katika mamlaka hiyo, Dk. Mpango pia alisema anapendekeza kufuta tozo ya ukaguzi wa viwanda vya samaki iliyokuwa inatozwa kati ya Sh. 200,000 na 250,000, tozo ya ukaguzi wa maduka mapya ya samaki Sh. 50,000 na tozo ya leseni ya mwaka ya biashara kati ya Sh. 50,000 hadi Sh. 300,000.

INAENDELEA UK.26



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakifuatilia kupitia matangazo ya televisheni, wakati Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiwasilisha Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2019/2020, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Ada leseni udereva juu, mawigi kutozwa ushuru

**Na Mwandishi Wetu**

ADA ya leseni ya udereva inatarajiwa kupanda kutoka Sh. 40,000 hadi 70,000 kuanzia Julai mwaka huu, baada ya serikali kupendekeza ongezeko hilo bungeni.

Akiwasilisha bungeni jana hotuba kuhusu mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema serikali pia inapendekeza kuongeza muda wa leseni hiyo kutoka miaka mitatu ya sasa hadi miaka mitano.

Alisema anapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usalama Barabarani, ili kuongeza muda wa leseni za udereva kutoka miaka mitatu sasa hadi miaka mitano na kuongeza ada hiyo pamoja na kuongeza ada ya usajili wa magari kutoka Sh. 10,000 ya sasa kwenda 50,000.

Waziri huyo pia alisema mapendekezo hayo yanalenga kuongeza ada ya usajili wa pikipiki za matairi matatu kutoka Sh. 10,000 hadi 30,000 na pikipiki kutoka Sh. 10,000 hadi 20,000.

Alisema lengo la mapendekezo hayo ni kupunguza gharama za kuchapisha leseni kwa kipindi cha miaka mitatu kwa kuwa leseni hizo zinaweza kudumu zaidi ya miaka mitano.

Alisema marekebisho hayo pia yanalenga kuoanisha gharama za uchapishaji wa leseni na kipindi cha leseni husika.

"Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya serikali kwa kiasi cha Sh. bilioni 18.147," alisema.

**TOZO KWENYE MAWIGI**

Dk. Mpango pia alisema anapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nywele bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na asilimia 25 kwenye nywele zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na kwamba lengo la hatua hiyo ni kuongeza mapato ya serikali.

Pia, anapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye bidhaa za mabomba na vifaa vya plastiki vinavyotumika kwenye ujenzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kuwa hivi sasa kuna viwanda vingi vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza mahitaji nchini.

Hatua hii itahusisha bidhaa za mabomba ya plastiki zinazotambuliwa na kwamba lengo la kuanzisha ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa hizo ni kulinda viwanda na kuongeza fursa za kazi, ajira na mapato ya serikali.

# Mafanikio 17 ya awamu ya tano

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amelieleza Bunge mafanikio 17 yaliyopatikana katika miaka mitatu na nusu ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Dk. Mpango alibainisha mafanikio hayo alipowasilisha bungeni jijini Dodoma jana taarifa kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20.

Katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya utawala wa serikali ya awamu ya tano (2016-2017-2017-2018) yamepatikana mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo.

UKUAJI WA UCHUMI

Waziri Mpango alisema katika kipindi hicho cha miaka mitatu na nusu uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.9 na mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kuwa katika wastani wa kiwango cha tarakimu moja, chini ya asilimia tano.

**RELI**

Dk. Mpango alisema ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge unaendelea, akibainisha kuwa awamu ya kwanza ya Dar es Salaam–Morogoro–Makutupora (Km 300) utekelezaji umefikia asilimia 48.9 na Morogoro–Makutupora (Km 422) umefikia asilimia 7.12.

Alisema taratibu za ujenzi kwa sehemu za Makutupora–Tabora (Km 294), Tabora-Isaka (Km 133), Isaka-Mwanza (Km 249), Isaka–Rusumo (Km 371), Tabora-Kigoma (Km 411), Keza–Ruvuba (Km 36) na Kaliua–Mpanda–Karema (Km321) unaendelea.

**ATCL**

Waziri huyo alisema mpaka sasa, ndege sita zimenunuliwa na kwamba kutokana na kuboreshwa kwa Shirika la Ndege (ATCL), idadi ya abiria imeongezeka kutoka 49,854 mwaka 2015/16 hadi 242,668 mwaka 2018/19. Alisema shirika pia limeongeza idadi ya miruko kutoka 49,854 mwaka 2015/16 hadi 3808 mwaka huu wa fedha. "Pia serikali imefanikiwa kuongeza idadi ya mikoa iliyofikiwa kwa huduma kutoka mitatu hadi 11, kuongezeka kwa idadi ya vituo vya nje kutoka kimoja (Hayaya-Comoro) hadi vituo vitano(Hahaya, Bujumbura, Entebbe, Harare na Lusaka)," alisema.

**STIEGLER'S GORGE**

Dk. Mpango alisema serikali imepata mkandarasi wa mradi wa kufufua umeme utokanao na nguvu ya maji katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge, ambaye ni Kampuni ya Arab Contractors na Elsewed Electric S.A.E kutoka Misri.

"Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha njia ya kusafirisha umeme wa MW nane yenye msongo wa Kv 33 Msamvu, Morogoro hadi eneo la mradi yenye urefu wa Km 170," alisema.

**BOMBA LA MAFUTA**

Dk. Mpango alisema mafanikio yaliyopatikana katika mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania), ni kukamilika kwa tathmini ya fidia kwa maeneo ya kipaumbele na eneo lote la Mkuza.

INAENDELEA UK.26

# Kada wa Chadema auawa kwa risasi

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mwenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, Lucas Lihambalimu, ameuawa kwa kupigwa risasi akiwa nyumbani kwake na watu wasiojulikana.

Katibu wa Chadema Mkoa wa Morogoro, Barnabas Okola, aliiambia Nipashe jana kuwa Lihambalimu aliuawa usiku wa kuamkia juzi na watu hao ambao walifika nyumbani kwake saa nane usiku.

Alisema watu hao ambao idadi yao haijajulikana walifika nyumbani kwa katibu huyo na kugonga mlango walipofunguliwa, walitoa silaha na kumfyatulia kichwani.

"Watu hawa walikwenda nyumbani kwake huko Kata ya Mkimbira saa nane usiku walimgongea na alipotoka ndipo walipompiga risasi kichwani na kufariki hapohapo na wao kutokomea kusikojulikana," alisema.

Alisema hadi jana jioni walikuwa hawajapata taarifa yoyote kama marehemu alikuwa na mgogoro na mtu. Okola alisema mwaka 2013 Lihambalimu aliwahi kupigwa mapanga kichwani wakati wa uchaguzi mdogo wa udiwani. "Hatufahamu kama ni watu haohao wamerudi kwa mara nyingine au la, kwa sasa tunasubiri uchunguzi wa tukio hilo na mwili wake umezikwa leo (jana),"alisema.

Alipotafutwa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, (SACP), Wilbroad Mutafungwa, alisema hakuwa na taarifa hizo kwa kuwa hakuwa ofisini kutokana na kuumwa.



Rais John Magufuli akifurahi na wabunifu wa umeme wa maji kutoka mkoani Njombe, John Akane Mwafute (Mzee Pwagu) na Jailosi Ngairo aliowaita Ikulu, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwapongeza na kuwapa kifuta jasho cha Sh. milioni tano. **PICHA: IKULU**


BANK OF TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA TAWI LA ARUSHA

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

BENKI KUU YA TANZANIA TAWI LA ARUSHA INATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI SU 35499 LAND ISUZU PICKUP. YEYOTE ATAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA IMETOLEWA KITUO CHA POLIS KWA KUMB. **NAMBA AR/RB/5697/2019**

215272701


# Daftari wapigakura kuboreshwa Julai

**Na Enock Charles**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kuanza uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki kwa awamu ya kwanza kuanzia Julai, mwaka huu.

Akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, alisema uboreshaji huo utawahusu wapigakura wapya waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi na wale watakaotimiza umri huo siku ya uchaguzi mkuu ujao.

"Uboreshaji wa safari hii hautahusu wapigakura wote walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura mwaka 2015 bali utawahusu wapiga kura wapya," Jaji Kaijage alisema. Akitaja makundi mengine yatakayohusika na uboreshaji huo ni wale watakaoboresha taarifa zao kama vile waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika, wanaorekebisha upya taarifa zao na wale waliohama maeneo yao ya awali ya uchaguzi na kuhamia mengine.

Tume pia ilitoa orodha kwa viongozi na wawakilishi wa vyama vya siasa ya vituo vilivyohakikiwa na tume hiyo vitakavyotumika kuandikisha wapigakura na uhakiki liliongeza vituo 37,407 kutoka vituo 36,549 Tanzania Bara na vituo 407 kutoka vituo 380 Zanzibar. Sambamba na kazi hiyo, NEC kwa kushirikiana na asasi za kiraia itatoa elimu ya mpigakura kwa kutoa vibali kwa baadhi ya Asasi kwa ajili ya kutoa elimu kwa mara ya kwanza wakati wa uboreshaji wa daftari.

Akitoa ufafanuzi kuhusu uboreshaji wa daftari hilo ambao hutakiwa kufanyika mara mbili kabla ya uchaguzi mkuu, Jaji Kaijage alisema kazi hiyo kwa mara ya pili utafanyika baada ya kukamilika kwa uboreshaji awamu ya kwanza.

"Jibu sahihi kuhusu ni lini tume itafanya uboreshaji wa daftari la wapigakura awamu ya pili, jibu lake ni pale uboreshaji wa awamu ya kwanza utakapokamilika," alisema.


***Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-***

- ***Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=***
- ***Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=***
- ***Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima***
- ***Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku***

215227501



## HABARI KITAIFA

### KESI YA AVEVA

# Shahidi adai kupokea nyaraka za kontena za nyasi bandia

**Na Hellen Mwango**

MENEJA uendeshaji wa kampuni ya kutoa mizigo Wafem Tanzania Ltd, Jovin Kalinga, amedai mahakamani kwamba katika kesi ya kutakatisha Dola za Marekani 300,000 inayowakabili Rais wa klabu ya Simba, Evance Aveva na wenzake wawili, kwamba alipokea nyaraka za kutoa bandarini kontena tatu za nyasi bandia za klabu hiyo.

Kadhalika amedai kabla ya kupokea nyaraka hizo kutoka kwa mkurugenzi wa kampuni yao, alipata taarifa ya kazi hiyo kutoka kwa mfanyabiashara Zakaria Hans Poppe.

Meneja huyo ambaye ni shahidi wa tano wa Jamhuri alitoa ushahidi wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Alidai kuwa anamfahamu Hans Poppe kwa sababu alishafanya naye kazi ya kumtolea mizigo bandarini.

Alidai kuwa hakumbuki siku, lakini Hans Poppe alimweleza kwamba kuna kazi klabu ya Simba ya kutoa makontena matatu hivyo akauone uongozi wa klabu hiyo.

Akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, shahidi alidia kuwa alimpelekea taarifa bosi wake Mkurugenzi Levison Kasulwa, aliwasiliana na uongozi wa Simba.

"Bosi wangu aliniita akanikabidhi jalada la klabu hiyo nilifanyie kazi nilipokwenda bandarini nilipigiwa simu na Makamu Mwenyekiti wa Klabu Salimu akanifahamisha kwamba makontena hayo ya nyasi bandia yamezuiliwa na Takukuru kwa ajili ya uchunguzi." Alidai Kalinga.

Alidai kuwa katika nyaraka za klabu, mzigo ulionyesha una thamani ya Dola za Marekani 41,000 na makadirio ya kulipa kodi ilikuwa Sh. milioni 82.

Baada ya mwezi mmoja tangu mzigo umezuiliwa bosi wake alipigiwa simu wakaitwa kwenda kujieleza Takukuru kuhusu nyaraka za kutolea mzigo huo.

Hata hivyo, wakati wakihojiwa na ofisa wa Takukuru Frank kuhusu mzigo wa klabu hiyo, walikiri kufahamu nyaraka za kutoa kontena tatu zenye mali ya Dola za Marekani 41,000.

Aidha, ofisa huyo aliwahoji kuhusu nyaraka inayoonyesha thamani ya mali ya Dola za Marekani zaidi ya 100,000, walikanusha kufahamu.

Shahidi alidai kuwa anawafahamu pia Kaburu na Aveva kwa sababu nyakati tofauti aliwasiliana nao kuhusu masuala ya kutathmini na kupata punguzo la kodi.

Kesi hiyo itaendelea Juni 19, mwaka huu kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri.

Katika kesi ya msingi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shadrack Kimaro alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016, Aveva na Kaburu walikula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya ofisi.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva na Kaburu walifanya matumizi mabaya ya madaraka kwa kuandaa hati ya kuhamisha Dola za Marekani 300,000 kutoka akaunti ya Klabu ya Simba benki ya CRDB tawi la Azikiwe kwenda akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays tawi la Ohio. Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la tatu, Machi 15, mwaka 2016 Aveva na Kaburu, wote kwa pamoja walighushi fomu ya kuhamisha fedha ya tarehe hiyo wakionyesha kwamba Klabu ya Simba inalipa deni la Dola za Marekani 300,000 kwa Rais wake Aveva.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo TTB kwa kujiongeza

**BODI** ya Utalii Tanzania (TTB) imejipambanua kufanya ziara ya utangazaji wa utalii (roadshows) nchini China.

Lengo likiwa ni kuhakikisha inavutia hatimaye kuwashawishi watalii kutoka nchini humo kuja kutembelea vivutio vilivyopo nchini, hivyo kujiimarisha katika soko la utalii.

Hatua hii ni jambo la kupongeza kwa kuwa litasaidia kukuza uchumi kwa kuwa pia imelenga kuwahamamisha wawekezaji waliopo katika nchi hiyo nao kuja kuangalia fursa zilizopo na kuwekeza.

Mwenyekiti wa Bodi ya TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, amesema kuwa ziara hiyo ya wiki moja inaanza Juni 19 hadi 26, na kuwa inafanywa katika miji minne ya China ambayo ni Beijing, Shangha, Nanjig, Changsha hatua hii ni kuhakikisha Tanzania inaongeza sehemu ya umiliki wa soko kwenye soko la utalii China.

Katika ziara hiyo TTB itaambatana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi na ya umma ikiwamo TANAPA, NCAA, Wakala wa Huduma za Misitu, Makumbusho ya Taifa Idara ya Mambo ya Kale, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Wadau hawa ni muhimu nao watashiriki katika kusaidia kuelezea kwa kina yaliyomo kwenye idara zao, mfano Idara ya Wanyamapori kushawishi kwa maelezo ya sifa za ziada za wanyama waliopo Tanzania kama vile faru fausta.

TTB imejiongeza kutumia fursa hiyo baada ya Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) na vyanzo vingine mbalimbali duniani kubainisha kuwa soko la watalii kutoka China linaendelea kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya watalii na mchango katika uchumi wa dunia.

Kwa mujibu wa Jaji Mihayo, TTB na wadau wake waliona fursa kubwa ya kuongeza jitihada za kuwavutia watalii zaidi kutoka China, na nchi hiyo Novemba 2018 iliratibu ziara kubwa ya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania.

Kwamba, watatumia nafasi hiyo kutangaza safari za ndege mpya za Air Tanzania ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, hivyo watalii wanaohitaji kuja nchini wanaweza kutumia usafiri huo. TTB imeonyesha umakini kwa kutathmini ziara ya awali iliyofanyika katika miji ya Beijing, Shanghai, Chengdu, Guangzhou na Hong Kong, ambayo ilizaa matunda kwa kundi la watalii zaidi ya 300 kuja nchini na kutembelea vivutio vya utalii mwezi Mei 12 hadi 16.

Pamoja na kwamba mafanikio hayo yalichangiwa pia na makubaliano kati ya TTB na Kampuni ya Touchroad International Holding Group waliyoingia Novemba 2018 kuleta watalii 10,000 kutoka China kwa kipindi cha mwaka 2019.

Utangazaji wa vivutio umefanywa kwa namna tofauti ukiwakumbuka pia na watalii wa ndani ambapo kuna matangazo yamewekwa hadi kwa lugha ya Kiswahili ili ieleweke kwa haraka na kwa wananchi wa kada tofauti.

Mfano tangazo la Mangi anayehojiwa kufunga duka lake baada ya kulifunga siku nne, ambapo anajibu kuwa alikwenda kutalii na wanae katika Ziwa Manyara kuna daraja moja zuri.

Mteja wake anamshangaa Mangi kuwa je amekuwa mzungu hadi aendee kutalii, anamjibu kuwa Watanzania nao wameamua kwenda kutalii kwenye hifadhi wanataja hadi viingilio 2,360 mtu mzima 11,800.

Sote tunaelewa kuwa kwa muda mrefu TTB imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi hususan ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii.

Tunaamini kuwa bodi hiyo baada ya kuongezewa muda wa miezi mitatu na Rais John Magufuli hivi karibuni, itachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha inapata fedha za kutangaza vitutio vyetu.

Kikubwa zaidi ni serikali kuiwezesha TTB kwa bajeti ili malengo yake yatekelezwe kwa ufanisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tukae chini kutafakari upya kuhusu ajira hizi za watoto

Na Sabato Kasika

**UJUMBE** wa mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ajira kwa Watoto Duniani yaliyofanyika siku chache zilizopita, unatamka:"Watoto wasifanye kazi shambani, bali wafanyie kazi ndoto zao".

Hapo ina maana kwamba watoto waachwe wakue na kukuza ndoto zao kupitia njia mbalimbali, ikiwamo elimu, badala ya kuwaingiza kwenye ajira na kujikuta wakikwama kutimiza ndoto zao.

Kila siku ya Juni 12 ya mwaka, Maadhimisho ya Kupinga Ajira kwa Watoto Duniani hufanyika na inaelezwa kuna jumla ya watoto milioni 150 wanaofanyishwa kazi duniani kote na hawapati nafasi ya kuhudhuria shule.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Anna Henga kwa vyombo vya habari, anayesema wengi wanatumikishwa katika sekta mbalimbali.

Aidha, anasema kuna aina nyingi za ajira kwa watoto, ikiwamo kufanya kazi shambani na viwandani na wengine wanatumika katika vita, wakilazimishwa kuomba maslahi ya wengine.

"Wengine huhusishwa katika aina mbaya zaidi za ajira kwa watoto kama kufanyishwa biashara za ngono, kushirikishwa katika biashara za dawa za kulevya na kazi nyingine zisizofaa," anadokeza Anna.

Anasema nchini ajira nyingi za watoto ziko katika mifumo ya wafanyakazi wa majumbani, mashambani, ombaomba na biashara za ngono.

Inaelezwa, ajira hizo zinawaathiri watoto, kwa vile wanashindwa kukua kiakili, wanashindwa kuhudhuria masomo na kwamba Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inamtafsiri mtoto kuwa ni yeyote mwenye umri wa miaka chini ya 18.

Pia, inatoa ufafanuzi kuwa ukatili kwa watoto unajumuisha kuwaajiri katika namna ya kuwanyonya watoto.

"Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mtoto kinaeleza kuwa mtoto hatahusishwa katika kazi yoyote ambayo inaweza kumsababishia madhara kiafya, kielimu, kiakili, kimwili na katika ukuaji wake," anasema.

Anasema, ni kosa la jinai kumuajiri mtoto katika kazi zisizofaa na zenye madhara kama ilivyoelezwa na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, inayoweka umri wa chini kaatika ajira ni miaka 14.

Anna anafafanua kuwa kazi hizo hazitakiwi kuathiri mahudhurio ya mtoto shuleni na haki nyinginezo. Lakini anasema, nchini watoto wanafanyishwa kazi na hawahudhurii shule, hali inayowafanya wakose haki ya kupata elimu.

Anaweka wazi kuwa mtoto aliyehitimu elimu ya msingi na ana umri wa miaka 14 na zaidi anaruhusiwa kufanya kazi, lakini isizidi saa sita.

Mchambuzi huyo analamika kuwa, iko kinyume kwamba watoto wengi hufanyishwa kazi zaidi ya muda huo na jamii haitambui kuwa wanavunja haki za msingi za watoto.

Kwa ujumla ni kwamba mkurugenzi huyo anagusia mambo mengi, huku mkazo wake ukiwa ni kutaka watoto waachwe watimize ndoto zao, pia wapate muda wa kucheza na kushiriki na wenzao katika ukuaji.

Hapo inaelezwa jamii haiwezi kukwepa majukumu na badala yake inapaswa kushiriki kikamilifu kukomesha ajira kwa watoto, zinazochangia kuwafanya wakose haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Kama anavyosema Anna, kwamba siyo jambo jema jamii ikiwaacha watoto wakiajiriwa kama wafanyakazi wa ndani, shambani, viwandani au kufanyishwa biashara za ngono, hivyo kila mmoja anapaswa kukemea hilo.

Imekuwa ikielezwa kuwa, mifarakano katika ndoa ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuwapo kwa watoto wa mitaani na wanaojiingiza kwenye ajira zisizofaa.

Inaelezwa kwamba iwapo mifarakano katika ndoa itakoma, kuna uwezekano wazazi wakawa na nafasi nzuri ya kulea na kuwalinda watoto wao, ili watimize ndoto zao, itakuwa rahisi kushirikiana katika kuwatimizia mahitaji na watahudhuria masomo shuleni.

Vilevile tatizo hilo la kuwapo ajira kwa watoto, inapaswa kuwa fundisho kwa jamii, ili ishituke na kuchukua hatua zinazostahili kuzingatia malezi yanayotakiwa na itakuwa imeisaidia serikali kupambana na ajira hizo.

HABARI KITAIFA

# Wanandoa wadaiwa kuua mtoto kwa kumchuna ngozi

**Na George Tarimo,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa linawashikilia watu wawili, mume na mke kwa tuhuma za kumchuna ngozi kwenye paji la uso mtoto wao wa kumzaa na kusababisha kifo chake.

Mtoto huyo Laurent Kitangwila, alikuwa na umri wa miezi miwili.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alisema tukio hilo lilitokea Juni 10, mwaka huu, majira ya saa sita mchana katika Kijiji cha Kinegembasi, Kata ya Kitandula Tarafa ya Kisanga, Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

Kamanda Bwire aliwataja wazazi wa mtoto huyo kuwa ni Patson Kitangwila (27) na mkewe Neema Nzilo (31), mkulima wa Kinegembasi.

"Kwa mujibu wa maelezo yao wakiwa wamelala na mtoto huyu waliamka asubuhi wakakuta amekatwa na kitu chenye ncha kali (kuchunwa ngozi kwenye paji la uso hadi puani) na akiwa tayari amefariki, lakini wamekuja kutoa taarifa majira ya saa sita mchana katika tukio hili tumewakamata wazazi wote wawili na tunaendelea na uchunguzi," alisema Bwire.

Alisema kuwa katika ukaguzi wa tukio hilo, jengo na nyumba walimokuwa wamelala, hakuna sehemu yoyote iliyovunjwa wala dirisha lililovunjwa na kila kitu kilikuwa kiko sawa na hakukuwa na damu yoyote pale alipokuwa amekatwa au pale alipolala kitandani na ndiyo sababu wazazi nao wameshikiliwa kusaidia polisi.

Kamanda alisema kwa taarifa walizopata hadi sasa ni kwamba baada ya mahojiano ya awali inasemakana usiku ule baba alitoka na mtoto akaenda naye sehemu isiyojulikana.

Alisema kuwa jeshi hilo linaendelea na ufuatiliaji na wamekamata watu watano wakiwamo waganga wa kienyeji wawili hivyo wanaendelea uchunguzi nini kilichojiri kwa sababu hadi sasa tukio linawapa utata.

# Rufani waliofungwa maisha yakwama

**Na Hellen Mwango**

RUFANI ya washtakiwa watatu kati ya wanne waliohukumiwa kifungo cha maisha gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kuchoma moto Kituo cha Polisi Bunju, imeshindwa kuanza kusikilizwa baada ya majalada ya kesi kufunguliwa tofauti.

Majalada ya watuhumiwa hao yamefunguliwa tofauti na kusababisha mengine kushindwa kufikishwa kwenye kikao cha Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kilichoketi jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Jana Wakili wa Serikali, Sadah Mohamed, alidai mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Clecensia Kasongo, kwamba rufani hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kusikilizwa.

Hata hivyo, alidai kuwa jalada la mwenendo wa kesi alionao siyo wa mshtakiwa aliyekuwa mahakamani hapo, bali anayo ya mrufani Abrahamu Mlinga.

Aliomba mahakama kutoa muongozo ili kufahamu nini kifanyike kwa sababu rufani iliyoko mbele yake ilikuwa inamhusu Juma Konzo.

Wakili wa washtakiwa hao Profesa Abadallah Safari, alidai kuwa hati ya wito mahakamani aliyonayo ni ya washtakiwa watatu ambao ni Yusuph Sungu, maarufu kama Mayuku ambaye jana hakuwapo mahakamani, Juma Konzo na Abrahamu Minga.

Hakimu alisema mahakama yake inaahirisha kusikiliza rufani mpaka Juni 17, 2019.

Mapema Februari, mwaka huu, Mahakama ya Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, iliwahukumu kifungo cha maisha washtakiwa wanane baada ya kutiwa hatiani katika kesi ya kuchoma moto kituo cha polisi cha Buju A na washtakiwa 10 waliachiwa huru.

Waliohukumiwa ni Yusuph Sugu (40), Juma Konzo (32), Rashid Liwima (29), Baraka Nkoko (23), Abuu Issa (36), Abraham Mninga (23), Veronica Ephraem (32) na Ramadhan Said (22).

Walioachiwa huru ni Mrisho Majaliwa (30), Hamis Ndege (37), Seleman Gwae (33), Meng'enya Antony (28), Rehema Hussein (32), Rajab Ally (25), Ally Athuman (24), Amina Matipwili (33), Gubila Temba (51) na Mariam Honza (44).

Katika kesi ya msingi, walidaiwa kuwa Julai 10, 2015 walichoma kituo cha polisi.

# Mama wa mtoto mwenye ualbino aliyetekwa aomba ulinzi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKATI watu wenye ualbino wakiadhimisha siku yao jana, mama wa mtoto mwenye ualbino, Agness Joseph, ambaye mtoto wake Debora Joseph (6), alitekwa na baadaye kupatikana kwa juhudi za wananchi, ameomba serikali kuwaongezea ulinzi kutokana na kuendelea kwa vitisho dhidi ya watu hao.

Agness mkazi wa Kijiji cha Magoweko, wilayani humo, aliwasilisha ombi hilo kwa waandishi wa habari walioambatana na Shirika la Kimataifa lisilo la Kiserikali la Kutetea Usalama, Ustawi na Watu wenye Ualbino (Under the Same Sun), lilotembelea wilaya hiyo kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kuwalinda watu wenye ualbino.

Alisema licha ya tukio la mtoto wake Debora kutekwa mwaka 2017 akiwa nyumbani kwake na mmoja wa wakazi wa eneo hilo na baadaye kupatikana akiwa mzima kutokana na jitihada za wananchi, huku mtuhumiwa akiwa ametoweka kusikojulikana, ameiomba serikali kuangalia namna ya kuimarisha ulinzi wa watu hao wenye ualbino.

"Wakati mwingine nashindwa kutembea na mtoto wangu kwenye maeneo tofauti kutokana na kuhofia usalama wake, hivyo tunaomba serikali kutuimarishia ulinzi," alisema Agness.

Pia aliomba serikali kuendelea kuhamasisha jamii kuwaona watu wenye ualbino kuwa ni sehemu ya jamii kama wengine ili kuondoa

INAENDELEA UK. 8


## TANZANIA FOOD AND DRUGS AUTHORITY

TFDA
Tanzania Food & Drugs Authority

**PRE-QUALIFICATION FOR SUPPLIERS OF LABORATORY EQUIPMENT, CHEMICALS, REFERENCE STANDARDS, MEDIA, GLASSWARE, CONSUMABLES AND MAINTENANCE OF LABORATORY EQUIPMENT FOR FINANCIAL YEAR 2019/2020**

**INVITATION FOR PRE-QUALIFICATION**

**Date: 14/06/2019**

1. The Tanzania Food and Drugs Authority (TFDA) has set aside funds in its budget to facilitate the Supply of various Laboratory Equipment, Chemicals, Reference Standards, Media, Glassware, Consumables, and Maintenance of Laboratory Equipment. It is intended to apply part of the proceeds of this fund to cover eligible payments under the contracts for which this prequalification is issued. It is expected that invitations to bid will be made in financial year 2019/2020.

2. Pre-qualification will be conducted through National Competitive Tendering procedures specified in Regulation 119 of the Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations– Government Notice 446 of 2013, as amended in 2016 and is open to all firms and voluntarily formed joint ventures.

3. Tanzania Food and Drugs Authority now invites sealed proposals for Pre-qualification of suppliers and Service Providers in the following categories:-

| LOT No. | DESCRIPTION |
|---|---|
| 1 | Suppliers of Laboratory Equipment |
| 2 | Suppliers of Laboratory Chemicals |
| 3 | Suppliers of Laboratory Reference Standards and Media |
| 4 | Suppliers of Laboratory Glassware and Consumables |
| 5 | Preventive Maintenance of Laboratory Equipment |

The prospective Suppliers and Service Providers may submit the Pre-qualification Document for one or more Lots.

4. Interested applicants may obtain further information from and inspect the Pre-qualification document at the Office of the Secretary, Tanzania Food and Drugs Authority Tender Board, 1st floor, Room No. 27, P.O. Box 77150, Off Mandela Road - Mabibo, Dar-es-Salaam, Tanzania, Tel.2450512/2450751, Fax 2450793 from 0900 – 1530 hours local time on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

5. A complete set of Pre-qualification documents in English may be purchased by interested applicants and voluntarily formed joint ventures on the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of [One Hundred Thousand Only (TZS. 100,000.00)]. The method of payment should be by Government Electronic Payment Gateway (GePG).

6. Applications for Pre-qualification should be submitted in one original plus two copies in sealed envelopes delivered to the Secretary either by hand or be sent by registered post so as to reach the Secretary, through the address in para 4 above on **Thursday 27th June, 2019** before 1400 hours local time and be clearly marked Pre-qualification for Suppliers and Service Providers for the year 2019/2020. Tenders sent by post must be registered.

7. Application for Pre-qualification in form of Telegraphic, Telex, Telefax and e-mail will not be accepted and those which will not be received and not opened in public at the public bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**ACTING DIRECTOR GENERAL**
**TANZANIA FOOD AND DRUGS AUTHORITY**

215273002

# Bajeti yabana, yapuliza

INATOKA UK. 2

halmashauri ni Sh. bilioni 765.5.

Dk. Mpango pia alisema serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 4.96 kutoka soko la ndani. Kati yake, Sh. trilioni 3.46 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na kiasi cha Sh. bilioni 1.5 sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

"Kwa lengo la kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu, serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 2.32 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara," alisema.

Alisema washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Sh. trilioni 2.78 ambayo ni asilimia nane ya bajeti.

"Misaada na mikopo hii inajumuisha miradi ya maendeleo Sh. trilioni 2.31, mifuko ya pamoja ya kisekta Sh. bilioni 199.5 na misaada na mikopo nafuu ya kibajeti Sh. bilioni 272.8," alisema.

**MATUMIZI**

Dk. Mpango alisema serikali inapanga kutumia Sh. trilioni 33.11 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo.

Alisema kuwa Sh. trilioni 20.86 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha Sh. trilioni 9.72 kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Serikali na Sh. trilioni 7.56 kwa ajili ya mishahara.

Alisema Sh. trilioni 3.58 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikijumuisha Sh. bilioni 460.5 kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya halmashauri.

Alibainisha kuwa serikali imetenga fedha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

"Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 12.25 sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ambao kiasi cha Sh. trilioni 9.74 ni fedha za ndani na Sh. trilioni 2.51 ni fedha za nje," alisema.

Alisema kiasi cha Sh. trilioni 2.48 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha reli ya kati ya kisasa (SGR), Sh. trilioni 1.44 ni kwa ajili ya mradi wa kufua umeme katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge na Sh. bilioni 450 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Na Sh. bilioni 288 ni kwa ajili ya elimu msingi bila ada. Aidha, serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, watoa huduma na makandarasi wa barabara, maji na umeme," alisema.

# Mwenye ualbino aomba ulinzi

INATOKA UK. 7

vitendo vya unyanyapaa na udhalilishaji badala ya kuyaachia mashirika yasiyo ya kiserikali pekee.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyarutanga, Kata ya Kisaki, Wilaya ya Morogoro, Said Masongela, aliiomba serikali na wadau mbalimbali kumsaidia mkazi wa kijiji hicho, Nasoro Msingili (69), mwenye ualbino na asiyeona aliyekatwa mkono Machi 10, 2017 na watu waliomvamia nyumbani kwake.

Akizungumza baada ya Shirika la Under The Same Sun kufika kijijini hapo kutoa elimu ya kuwalinda watu wenye ualbino, Mwenyekiti huyo alisema kwa sasa Msingili anaishi kwenye mazingira hatarishi kutokana na nyumba yake ya nyasi kuwa mbovu na anaishi na mke wake ambaye naye ni ajuza.

Masongela alisema kuwa msaada unaotolewa na serikali ya kijiji pamoja na wasamaria wema wengine wa kijijini hapo hautoshelezi mahitaji hivyo mara kadhaa mzee huyo amekuwa akilala na njaa na hata kunyeshewa na mvua kutokana na nyumba yake kuvuja.

Akieleza namna alivyovamiwa na watu na kukatwa mkono, alisema kuwa akiwa amelala na mke wake usiku wa manane ghafla alishtuka na kukuta amezingirwa na watu, huku wengine wakimshika mkono wa kushoto na alipojaribu kupiga kelele mmoja wa watu hao alimkata mkono na kukimbia nao.

Mzee Msingili alisema kuwa haoni, kwa kuwa hakuweza kuwatambua watu hao hata hivyo baadaye aliambiwa kwamba watuhumiwa waliomkata mkono wamekamatwa japokuwa mpaka sasa hajui kesi hiyo imefikia wapi kwa kuwa hajawahi kuitwa mahakamani, polisi wala kwa kiongozi yeyote.

## SHUKURANI




Sisi, familia ya marehemu Prof. Robert B.M. Mabele, tunatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki nasi tangu kumuuguza, kutwaliwa, maombolezo, na hatimaye kumpumzisha mpendwa wetu Prof. Robert B. Mabelle, "Kaka", "Bob" au "Uncle Bob" kama alivyojulikana na watu wake wa karibu, katika nyumba yake ya milele, makaburi ya Kinondoni Dar es Salaam.

Tunathamini ushiriki wenu wa hali na mali katika kufanikisha kumpumzisha mpendwa wetu kwa heshima zote alizostahili.

Tunatoa shukurani maalum kwa wafanyakazi hospitali ya serikali Iringa, hospitali aliyokuwa akitibiwa huko India, na hospitali za TMJ na Muhimbili (Mloganzila), Dar es Salaam kwa juhudi walizozifanya kujaribu kuokoa Maisha ya mpendwa wetu. Pia tunawashukuru jamii ya vyuo vikuu vya Ruaha (RUCU) na Dar es Salaam (UDSM) kwa ujumla wao, Uongozi wa kanisa la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, marafiki na wote waliosoma na kufanya kazi na mpendwa wetu katika maeneo mbali mbali, pia ndugu, marafiki na majirani wa ukoo wa Mabele katika ujumla wao kwa kujitoa kwenu kwa moyo katika kufanikisha yote kwa ajili ya safari ya mwisho ya mpendwa wetu, MUNGU awabariki sana.

Hatuwezi tumshukuru mtu mmoja mmoja, lakini kwa heshima kubwa tunawaomba wote mtambue shukurani hii kwenu.

Tutafarijika sana kwa uwepo wenu katika MISA YA SHUKRANI itakayofanyika katika Kanisa Katoliki la Mt. Anna, Hananasif Kinondoni, siku ya Jumamosi, Juni 15, 2019 saa nne kamili asubuhi na kufuatiwa na chakula cha mchana nyumbani kwa Bw. na Bibi Charles Yanga, Tabata Chang'ombe, Dar es Salaam.

"BWANA akubariki, na kukulinda; BWANA akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili; BWANA akuinulie uso wake, na kukupa amani." Hesabu 6:24-26

**"Ina thamani machoni pa Bwana Mauti ya wacha Mungu wake." Zaburi 116:15**
**FAMILIA YA MABELE**

115274302

Form 360b

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

Notice of Appointment of Liquidator: Voluntary Winding-Up: for insertion in Gazette Pursuant to section 360 of the Companies Act 2002

| | |
|---|---|
| Company Number | [illegible] |
| Company Name (In Full) | FERECK SAFARIS COMPANY LIMITED |
| Type of Liquidation | [members'] [creditors'] MEMBERS |
| Address of Registered Office | P.O. BOX 60112<br>DAR ES SALAAM,<br>TANZANIA. |
| Liquidator(s) name(s) | PHILEMON MWITA MATIKO |
| Liquidator(s) address(es) | P.O. BOX 60112<br>DAR ES SALAAM,<br>TANZANIA. |
| Date of appointment | 3[rd] JUNE 2019 |
| By whom appointed | FERECK SAFARIS COMPANY LIMITED |

Signed.................................... Date 03/06/2019

NAME IN BLOCK LETTERS PHILEMON MWITA MATIKO
(by each liquidator if more than one)

Signed.................................... Date....................

NAME IN BLOCK LETTERS....................

215275102

RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz @RadioOneStereo @RadioOneStereo @radioonetz

# Mama asimulia ndoa yake ilivyovunjika akiwania udiwani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Chibe, Manispaa ya Shinyanga, Sara Nyabuyaga, amesimulia kadhia alizokutana nazo wakati akigombea nafasi ya udiwani wa viti maalumu mwaka 2015 na kusababisha ndoa yake kuvunjika.

Alisema nafasi hiyo aligombea na wifi yake na alianza kupokea vitisho kutoka kwa familia ya upande wa mumewe, lakini hakukata tamaa na kuendelea kupiga kampeni, lakini uchaguzi ulipokaribia wifi yake huyo aliuvunja mji wake na kisha kunyang'anywa watoto na kwenda kuishi nao.

Nyabuyaga alitoa simulizi hiyo jana mjini hapa kwenye semina ya kuwajengea uwezo wanawake kushiriki kikamilifu kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu (2019), pamoja na uchaguzi mkuu ujao (2020), mafunzo yaliyotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP.

Alisema wanawake wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi pale wanapojitokeza kutangaza nia ya kugombea uongozi ikiwamo kubezwa, kuombwa rushwa ya ngono, kukosa ushirikiano ndani ya familia, kurogwa, pamoja na baadhi yao kufikia kuvunja mji kwa kuonekana kupingana na mume. "Wanawake wengi tunaogopa kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye chaguzi hizi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kwa sababu tunapigwa sana vita, mimi mwenyewe ni mhanga ambapo mwaka 2015 niligombea nafasi ya udiwani wa viti maalumu nikiwa na wifi yangu na kufikia hatua ya kunivunjia mji," alisema Nyabuyaga.

"Sikukata tamaa na uchaguzi ulipokaribia nikavamiwa nyumbani kwangu na kuibiwa magunia 18 ya mpunga pamoja na kupewa barua ya onyo nisiendelee kugombea tena, nikaamua kuendelea sababu wananchi walikuwa wakinitaka, ila kwa bahati mbaya jina langu likakatwa kwa nguvu na kupewa nafasi hiyo wifi yangu," aliongeza.

Aidha, alidai kwa mwaka huu (2019), ametangaza nia lakini juzi wamevamia tena nyumbani kwake na kupewa kitisho asijaribu kugombea nafasi hiyo ya udiwani wa viti maalumu kwa kuwa watamfanya kitu kibaya, hali ambayo amedai imemvunja moyo na hivyo atagombea nafasi ya uenyekiti wa mtaa wa Chibe.

Naye Mwanaharakati kutoka mtandao wa jinsia Tanzania TGNP, jijini Dar es Salaam, Natujwa Mvungi, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo ili kuwajengea uwezo wanawake pamoja na kuwapa ujasiri wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, waweze kuwa na sauti pamoja na kutatua matatizo yanayowakabili na kuondoa mfumo dume.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akipooza kiu yake kwa maji ya dafu katika eneo la Urafiki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rukwa kukuza biashara DRC, Burundi, Zambia

**Na Mary Geofrey,** RUKWA

MKOA wa Rukwa unatarajiwa kukuza biashara ya mazao ya chakula na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Zambia, kufuatia kukamilika kwa bandari ya kisasa ya Kabwe inayojengwa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa Sh. bilioni 7.498.

Wananchi wa mkoa huo wamekuwa wakisafirisha mchele, mahindi, maharage, unga na sukari kwenda nchi hizo kwa kutumia mitumbwi, lakini baada ya ujenzi wa bandari hiyo kukamilika watasafirisha kwa kutumia meli.

Meneja wa Bandari ya Kigoma ambaye pia anasimamia bandari zote za Ziwa Tanganyika, Ajuaye Msese, akizungumza na waandishi wa habari waliotembela bandari hiyo jana, alisema ujenzi wake umefikia asilimia 50 na unatarajiwa kukamilika Aprili 2020.

"Kama mnavyoona bandari hii tunayojenga ya kisasa, itaenda kufungua uchumi wa wakazi wa mkoa wa Rukwa, kwa sababu wanategemea sana biashara ya kuuza mazao yao katika nchi za Congo na Burundi," alisema Msese. Alieleza kuwa bandari ndogo iliyopo ina kina kifupi, hivyo haiwezi kupakia mizigo mingi na ya kutosha mahitaji ya nchi hizo, ndio sababu ya TPA kuanza kutekeleza mradi huo.

Msese alisema mbali na kujenga gati la kisasa lenye kina kirefu, pia wanajenga barabara na maegesho ya magari unaotekelezwa na Mkandarasi Sumry's Enterprises Ltd kwa gharama za TPA.

Alisema mradi huo pia unajumuisha jengo la kupumzikia abiria, jengo la mgahawa, ghala la kuhifadhia mizigo, nyumba za wafanyakazi na uzio.

Msese alisema mbali na miradi hiyo pia wamejenga ofisi za taasisi za serikali katika bandari hiyo na zote nchini ili kudhibiti uingiaji wa bidhaa feki na wahamiaji haramu.

Alisema Mamlaka ya Bandari inafanya kazi na Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Shirika la Viwango Tanzania(TBS) ili kudhibiti uhalifu katika mipaka hiyo. Naye mfanyabiashara wa kusafirisha mizigo kutoka Kabwe kwenda Kigoma na nchi za DRC na Burundi, Mohamed Nasoro, aliipongeza TPA kwa kuanzisha mradi huo na kusema kuwa utasaidia kupunguza adha walizokuwa wanapata za kusafirisha mizigo michache kwenda katika nchi hizo.

Alisema pia kutokana na bandari wanayotumia sasa kuwa na kina kifupi wanapata hasara ya kuangusha mizigo kwenye maji wanapoitoa nchi kavu kwa mitumbwi kwenda kuipandisha kwenye boti kubwa katikati ya maji.

Naye kibarua katika ujenzi wa bandari hiyo, Ally Rashid, aliishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huo ambao umemsaidia kupata ajira ya muda na kuweza kujikimu kimaisha.

# Waziri aionya Tarura

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema atawatumbua Wakala wa Barabara wa Mijini na Vijijini (Tarura) kwa kitendo cha kukata barabara na kuziacha muda mrefu bila kuzikarabati.

Warizi Jafo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifanya ukaguzi wa barabara na soko la Kijichi chini ya Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP), katika Wilaya ya Temeke.

Alisema tayari alishatoa maelezo mkoani Dodoma kuhusiana na wataalamu ambao wanakata barabara na kuziacha hadi miezi miwili bila matengenezo na anaendelea kupokea malalamiko ya kero hiyo.

"Nimetoa maelekezo kuwa kama hakuna bajeti ya kurekebisha barabara ni bora wasiikate kabisa tunatarajia barabara iliyokatwa kiboksi isizidi wiki moja iweze kuzibwa," alisema.

Aliongezea kuwa: "Wengi wamelalamika, wengine matairi ya gari yamekatika katika hizo barabara, natoa maelekezo yangu kwa upande wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), kuhakikisha barabara zote zilizokatwa ndani ya wiki moja ziwe zimerekebishwa," alisema.

Aidha, alisema kwa barabara ambazo ni za Wakala wa Barabara (Tanroad), kwa kuwa zipo chini ya waziri mwenzake na wanashirikiana, hivyo barabara zote zilizokatwa wataalamu kuhakikisha zinatengenezwa. "Haitakuwa vizuri unakata barabara ndani ya miezi miwili hadi miezi mitatu haijatengenezwa, Rais John Magufuli hili halipendi, lile eneo langu wale wa Tarura wakishindwa kurekebisha nitawatungua wale wa Tanroad nitawaachia kaka yangu Kamwele ashughulike nao," alisema.

Jafo alisema atakapopatiwa taarifa tena kuhusiana na suala hilo lazima awatungue kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo.

Alisema awali alitoa agizo hilo ndani ya wiki moja walirekebishe kwa sasa anaona ugonjwa umejirudia tena, hivyo ni marufuku kukata barabara na kuziacha kwa miezi miwili bila kurekebisha.

Aidha, alisema mradi wa DMDP unagharimu Sh. bilioni 660 ambao upo katika Wilaya ya Ilala, Temeke na Kinondoni.

Alisema, Wilaya ya Temeke mradi unaenda vizuri na kikubwa ifikapo Desemba kutakuwa na mabadiliko makubwa katika Jiji la Dar es Salaam.

"Watanzania waliotoka Dar es Salaam wakija mwakani itabidi tuwashike mikono kwa sababu mitaa waliyokuwa wameizoea itakuwa tofauti mfano mzuri ni leo ukifika Kijichi na Mbagala Kuu kama kuna mtu alitembea miezi sita inawezekana akakuta maeneo yapo tofauti hii ni kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya tano," alisema. Jafo aliwataka wananchi kutunza miundombinu ya barabara ikiwamo taa zitakazowekwa waache kuziiba.

Alisema katika eneo la Ujiji mkoani Kigoma wakati wanafanya kazi ya kubadilisha miundombinu kuna baadhi wameanza kuiba taa za barabarani.

"Tutafunga taa za kisasa kwa ajili ya barabara zetu tunatakiwa kutunza miundombinu yetu nimechukizwa na wizi wa taa za barabarani Kigoma."

Aidha, Jafo amemtaka mkandarasi anayejenga Barabara ya Temeke mwisho kwenda kwa Azizi Ally, kukamilisha ifikapo Agosti 30, mwaka huu na endapo atashindwa kutekeleza agizo hilo atakatwa fedha kwa mujibu wa mkataba.

# Vyanzo vikuu ajali vyatajwa

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imetaja vyanzo vikuu vitatu vinavyosababisha ajali za barabarani nchini.

Vyanzo hivyo ni pamoja na makosa ya kibinadamu ambayo huchangia kwa asilimia 76, ubovu wa magari asilimia 16 na mazingira ya barabarani kwa asilimia nane.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hamad Yusuf Masauni, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Manyinyi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema licha ya kazi nzuri ya waendesha bodaboda ya kurahisisha usafiri na kupunguza tatizo la ajira, bado kuna changamoto mbalimbali wanazosababisha kama vile ajali za mara kwa mara pamoja na wizi.

"Je, nini mkakati wa serikali wa kupunguza tatizo hilo? Na je, serikali haioni umuhimu wa kutofautisha adhabu ya waendesha bodaboda na ile ya magari makubwa kulingana na vipato vyao?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema makosa ya kibinadamu ni pamoja na uendeshaji wa kizembe au hatari, ulevi, mwendo kasi, uzembe wa waendesha pikipiki na uzembe wa watembea kwa miguu na sababu zingine.

Aidha, alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikitoa elimu kwa waendesha bodaboda namna nzuri ya utumiaji wa pikipiki ikiwa ni pamoja kuvaa kofia ngumu.

Pia alisema serikali imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara wa leseni kwa waendesha bodaboda, ili kupunguza wale waendeshaji wasio na leseni wanaoweza kusababisha ajali.

Hata hivyo, alisema serikali imekwisha liona hilo na kwamba kuna hatua mbalimbali zinaendelea kufanyika ili hatimaye adhabu zitofautiane kati ya waendesha bodaboda na wale wa magari makubwa.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alisema Jeshi la Polisi lina mpango wa kuboresha na kujenga vituo vya polisi katika ngazi za tarafa na kata.

Akijibu swali la Mbunge wa Mtera (CCM), Livingstone Lusinde, aliyetaka kujua serikali ina mpango wa kujenga kituo kikubwa cha polisi katika Jimbo la Mtera, Masauni alisema mpango huo wa serikali ni kutaka kujenga vituo hivyo nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha.

Alisema kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu katika maeneo mengine hakuna huduma ya vituo vya polisi ikiwamo kijiji cha Mvumi Misheni ambacho hakina kituo.

Alisisitiza kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kuhakikisha kuwa wananchi na mali zao wanaishi salama na kwa kushirikiana na wabunge wa majimbo yaliyoko barabara ya Iringa hadi Dodoma watahakikisha kituo kinajengwa kwenye eneo hilo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angela Kairuki (kushoto) akijadiliana jambo na Mbunge wa kuteuliwa, Anne Kilango, bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

## Wenyeviti wa mitaa na kata si waajiriwa

BUNGE limeelezwa kuwa wenyeviti wa vijiji na mitaa si watumishi wa umma, hivyo hawaajiriwi na kulipwa mishahara kama ilivyo kwa watendaji wa maeneo hayo.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Mjini(CUF), Maftaha Nachuma.

Katika swali lake, Nachuma alihoji serikali inasema nini juu ya umuhimu wa kuwalipa mishahara wenyeviti wa vijiji kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma.

Waitara alisema kutokana na kutolipwa mishahara viongozi hao huwalipa posho ambayo inatokana na asilimia 20 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

"Ulipaji wa posho ya viongozi hawa unategemea makusanyo ya kila halmashauri na serikali inatoa wito kwa halmashauri zote ikiwamo Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani," alisema.




**Na Augusta Njoji,** DODOMA

# Mwongozo waandaliwa kuhusu viwanda

SERIKALI imesema mwongozo wa kubainisha majukumu ya mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa sera ya viwanda unaandaliwa na kwamba hadi sasa viwanda 3,000 vimejengwa nchi nzima.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema katika kujenga Tanzania ya viwanda, Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa na mikakati ya muda mrefu.

"Je, mkakati wa Ofisi ya Rais, Tamisemi kujenga viwanda 100 kwa kila mkoa ni sehemu ya mkakati na umeainishwa kwenye waraka gani wa serikali ili kuwapa wananchi rejea ya pamoja ya kitaifa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Waitara alisema ujenzi wa viwanda 100 kila mkoa ni sehemu ya mikakati mbalimbali inayotekelezwa na serikali ya awamu ya tano kujenga uchumi wa viwanda uliofungamanishwa na maendeleo ya watu.

Alisema Ofisi ya Rais, Tamisemi imeandaa mwongozo wa kubainisha majukumu ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa katika utekelezaji wa sera ya viwanda.

Alibainisha kuwa lengo la mkakati huo ni kutoa hamasa kwa viongozi na wananchi kushiriki kikamilifu kuwezesha uwepo wa viwanda katika maeneo yao.

"Hivyo, mkakati huo haupaswi kutengenishwa na mipango mingine ya serikali inayohamasisha

# HABARI ARUSHA



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, (mwenye kilemba) akiwa na Waziri wa Afya wa Kenya, Sicily Kariuki (kushoto kwake), na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia kwake), wakipata maelezo ya matumizi ya moja ya maabara inayohamishika inayotumika kupima magonjwa ya mlipuko mipakani, wakati wa zoezi la kupima utayari wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kukabiliana na magonjwa hayo, katika mpaka wa Tanzania na Kenya, eneo la Namanga, mkoani Arusha juzi. **PICHA: OWM**

## Wakulima wa alizeti wapania kuacha mbegu za asili

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAKULIMA wa zao la alizeti mkoani Manyara wamekiri kuwa mbegu za asili za zao hilo hazina tija na haziwezi kuendana na mabadiliko ya tabia ya nchi, hivyo wameamua kuanza kulima mbegu ya kisasa ili wainuke kiuchumi. Hayo waliyasema jana katika Kijiji cha Orngadida Kata ya Qash, Halmashauri ya Babati, wakati wakizungumza siku ya mkulima shambani iliyoandaliwa na Shirika la Farm Africa na kiwilaya ilifanyika kijijini hapo.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Gallapo, Lohay Langay, alisema wakulima kuendelea kulima mbegu ya zamani ya alizeti haziwapatii faida bali watakuwa wanalima ili kujikimu pekee.

"Kwa kuwa Farm Africa wanahamasisha mbegu ya Hysun 33 ambayo inatoa mavuno mengi na sisi tunaenda kuhamasishana tuanze kuilima ili tujikwamue kiuchumi," alisema Langay.

Aidha, alisema mabadiliko ya tabia ya nchi yanawaathiri wakulima huku akitoa mfano msimu huu kuwa hali ni mbaya zaidi kwa wakulima waliopanda mbegu ya alizeti ya asili.

"Mfano mtu aliyepanda mbegu ya zamani anavuna gunia moja mpaka mbili, wakati mbegu ya Hysun 33 mkulima hata ukame ukitokea anavuna magunia zaidi ya hayo," alisema.

Katika kuhamasishana kilimo cha zao hilo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati, Nicodemus Tarimo, alisema mchango wa Farm Africa ni mkubwa na kuwataka wakulima kuacha kuchanganya mazao wanapolima ili waandae mazingira ya kuvuna kiasi kikubwa.

"Kilimo cha kuchanganya alizeti na mahindi ni cha hasara sana, wataalamu wetu wahimizeni mno wakulima kutochanganya mazao ili walime kwa tija," alisema Tarimo. Alisema wakulima wanatumia gharama kubwa, lakini wanachokipata ni kidogo hivyo vema kila mmoja kubadilika na kulima kisasa kwa kuzingatia ushauri wa Farm Africa.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Qash, Adelta Macha, alisema Farm Africa haiwagawii fedha, bali inawapa elimu na kusaidia baadhi ya mbegu, wakulima zaidi ya 170 waliopewa mbegu kwa ajili ya kupanda, lakini hawakupanda kwa sababu wengi wao waliogopa hali mbaya ya hewa.

Meneja mradi wa alizeti maendeleo endelevu wa Farm Africa, Tumain Elibariki, alisema mradi huo unaofadhiliwa na Agricultural Markets Development Trust, unalenga kuwaunganisha wakulima na masoko.

"Lakini tunajivunia mafanikio yetu kwa kuwa tumeshawafikia wakulima 7,000 kwa mkoa mzima na siri kubwa ya mafanikio haya ni kuwatumia wataalamu wetu ambao ndio nguzo kuu katika kuwasaidia wakulima na kuleta mapinduzi ya alizeti mkoani hapa na taifa kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake aliyekuwa mgeni rasmi siku hiyo Mhandisi wa Kilimo kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa, Norbet Kyomushula, alisema lengo la mradi huo ni kuwa na kilimo biashara ambacho ndicho kitawatoa kwenye umaskini.

Aliongeza kuwa ni vizuri wakulima wa alizeti wakajua kuwa soko lipo kwa kuwa nchi inaagiza mafuta ya kula nje ya nchi hivyo ni fursa kwa wakulima.

## Tanzania kutengeneza dawa za magonjwa mlipuko

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

NAIBU Waziri wa Mifugo, Abdallah Ulega, amesema kuwa kwa sasa Tanzania ina uwezo wa kutengeneza dawa ya kudhibiti baadhi ya magonjwa ya mlipuko katika taasisi ya TVI iliyopo Kibaha jijini Dar es Salaam, ikiwamo dawa ya ugonjwa wa kimeta ambayo imeonekana kuwa tishio kwa mifugo, wanyamapori na binadamu.

Alisema hayo kwenye ufunguzi wa majaribio ya udhibiti wa magonjwa ya milipuko hususani homa ya bonde la ufa (Rift valley fever), katika eneo la mpaka wa Namanga unaounganisha Tanzania na Kenya, utakaoendeshwa kwa siku nne na wanachama wa jumuiya hiyo.

Alisema wizara yake imejipanga vizuri dhidi ya magonjwa ya mlipuko kwa mifugo na zoezi hilo linaloendelea lipo chini ya Umoja wa Afrika Mashariki, lakini wanashirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha utayari wa nchi wanachama unatekelezeka.

"Hata sasa tumefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa kimeta ambao una athari kwa mifugo, wanyamapori na binadamu," alisema.

Alifafanua kuwa kuna wataalamu wa kutosha wanaoshughulikia magonjwa hayo yanapotokea chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na maafa na mifugo ya Tanzania ni salama kwa kuwa wanapatiwa chanjo mara kwa mara, lakini pia kuna wataalamu wa kutosha katika vituo hivyo vya pamoja (OSBP) na katika maeneo ya mkoani.

Alidai kuwa mifugo mingi ya Tanzania inauzwa nchi jirani ya Kenya na kuwataka wananchi jirani wa Kenya kuondoa hofu juu ya mifugo hiyo, kwa kuwa kabla haijapelekwa huko kibiashara inafanyiwa ukaguzi na vipimo mbalimbali na wataalamu na endapo mifugo ikibainika kuwa na ugonjwa hawezi kusafirishwa kibiashara kwenda nchi nyingine.

"Magonjwa haya yanatoka kwa mifugo kwenda kwa wanyamapori hadi kwa binadamu hususani kimeta, tumejipanga ipasavyo, tunayo taasisi inayojihusisha na utengenezaji wa dawa ya kimeta ikiwamo taasisi ya TVI iliyopo Kibaha," alisema Ulega.

Bahati Saitoti, mkazi wa Namanga Tanzania, alisema kuwa miezi michache iliyopita ugonjwa wa kimeta ulivamia katika eneo la Wilaya ya Longido, alishuhudia chanjo zikitolewa kwa wakati muafaka na kuiomba serikali kuongeza watumishi wa kutosha katika idara ya mifugo.

"Longido ni wilaya ya kifugaji, tunaomba serikali iongeze nguvu kazi kwa kuhakikisha dawa zinapatikana pamoja na wataalamu wakutosha ili yanapotokea magonjwa ya mlipuko waweze kutoa huduma kwa wakati," alisema Saitoti.

Hata hivyo, alieleza kuwa mifugo, wanyamapori na binadamu ni waathirika wakubwa wa magonjwa hayo na kuitaka serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kujikinga na magonjwa hayo kwa kuwa wengi wao hawajui njia za kujikinga.

"Kwa mfano kuna wananchi hawaelewi ugonjwa wa kimeta unavyoambukizwa kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu, mfugo anaweza akafa na binadamu akala nyama yake bila kujua inaathari, bado tunahitaji elimu yakutosha," alisema Saitoti.

## Kundi maalumu lanufaika mikopo ya halmashauri

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, imevipatia vikundi 71 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, Sh. milioni 230.8 ya mikopo kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ili kuwanyanyua kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Asia Ngalisoni, akizungumza jana alisema vikundi hivyo ni vya kata 14 vilivyonufaika na mkopo huo.

Ngalisoni alisema mkopo huo umenufaisha vikundi 71, vikiwamo 59 vya wanawake 1,531, vikundi tisa vya vijana 238 na vikundi vitatu vya wenye ulemavu 57.

Alisema hadi mwezi Mei mwaka huu, halmashauri hiyo imekusanya Sh. bilioni 1.7 ikiwamo mapato ya ndani na marejesho ya fedha za vikundi vilivyokopeshwa awali.

"Mfuko huu unawanufaisha wananchi waliojiunga katika vikundi vyenye shughuli za ujasiriamali au vinavyokusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati," alisema Ngalisoni.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema fedha hizo zinazotolewa Hazina bila riba, hivyo vikundi hivyo vinapaswa kuchukua mikopo hiyo na kurejesha kiasi kile kile walichokopa.

"Nitoe wito kwa vikundi vyote vilivyokopeshwa na halmashauri virejeshe fedha hizo kwa wakati ili wengine nao waweze kukopa na kujikwamua kiuchumi," alisema Chaula.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Jackson Sipitieck, alimpongeza Mkurugenzi wa halmashauri yake, Yefred Myenzi, kwa kusimamia ipasavyo mapato hadi kufanikisha utolewaji wa mikopo hiyo.

"Wakati halmashauri nyingine zikisuasua kufanikisha mikopo sisi Simanjiro tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwa tunatoa mikopo hadi fedha nyingine zimebaki," alisema Sipitieck.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alitoa wito kwa vijana wa eneo hilo kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa mwitikio wao bado ni mdogo.

"Zile fedha zenu vijana za asilimia nne mnazopaswa kupewa hamjazichukua hivyo vijana wa Simanjiro mnapaswa kubadilika ili mnufaike kupitia mikopo hii tunayoitoa," alisema Myenzi.

Katibu wa wenye ulemavu Mji mdogo wa Mirerani, William Orata, alisema kupitia mkopo waliopata wamefanikisha uanzishwaji wa mashine ya kusaga nafaka.

Mmoja kati ya wanawake walionufaika na mkopo huo, Susan Alanyamuna, alisema wametengeneza sabuni aina ya Sidai.





# Jela miezi 6 kutaka kuua mwanawe

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKAZI wa Kijiji cha Kilingi, Sanya Juu wilayani Siha, Elizabeth Mmari, amehukumiwa adhabu ya kifungo cha miezi sita jela, baada ya Mahakama ya Wilaya hiyo kumtia hatiani kwa kosa kujaribu kumuua mwanawe kwa sumu.

Mmari (20) alikuwa akikabiliwa na kosa la kujaribu kumuua mtoto wake wa siku tatu kwa kutaka kumnywesha sumu.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Siha, Jasmine Abdul, alisema mahakama imemwona Mmari ana hatia na inampa adhabu hiyo kutokana na dhamira aliyokuwa nayo ya kutaka kukatisha uhai wa mtoto huyo.

Hakimu Jasmine alisema baada ya mahakama kuridhika na ushahidi uliotolewa na watu wanne wakiwamo majirani zake, mshtakiwa anatiwa hatiani kwa dhamira ovu ambayo ni kinyume cha Kifungu cha 38, Sura ya 16 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, David Chisimba, kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo Novemba 2, mwaka jana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa huyo alimnywesha mtoto wake sumu aina ya 'Dip' akidai kushindwa kumlea kutokana na maisha magumu yanayomkabili.

Kwa sasa, mtoto huyo amepelekwa katika kituo kimoja cha kutunza watoto yatima kwa ajili ya malezi, baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu na kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mwendesha mashtaka huyo aliomba mahakama kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutokana na kukithiri kwa vitendo vya kikatili dhidi ya watoto.

Aidha, katika utetezi wake mahakamani hapo, mshtakiwa huyo alikiri kutaka kukatisha uhai wa mwanawe kwa sababu baba mzazi wa mtoto huyo, kumtelekeza na kukimbilia kusikojulikana.





Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo, akizungumza na wadau wa sekta ya mawasiliano wa kanda hiyo, wakati wa mkutano wa kupokea maoni, mapendekezo na kusikiliza kero zinazohusu utendaji wa mamlaka hiyo, uliofanyika jijini Mwanza jana. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Wawekezaji maji wawasili Wilaya ya Same

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAHANDISI wawili washauri wa miradi ya majisafi na salama kutoka Taasisi ya Rotary ya Ames Lowa ya Marekani, wamewasili katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kuanza mchakato wa uwekezaji katika sekta hiyo. Jana, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alithibitisha kuwa wahandisi hao wamekuja kuangalia maeneo ya uwekezaji kwenye sekta ya maji ili kusaidiana na serikali kutatua tatizo la huduma hiyo wilayani hapa.

"Nadhani inakuja ahueni kwa wananchi wa Same ambao wanakabiliwa na ukosefu wa maji kwa miongo kadhaa, baada ya Rotary Club ya Same na Rotary Club ya Ames Lowa ya Marekani kukubali kuja kuwekeza katika miradi ya maji ili kuwezesha wananchi kupata maji safi na salama," alisema.

Mradi unaotarajiwa kutekelezwa ni wa Mhezi ambao unafadhiliwa pia na Rotary, utahudumia vijiji vitatu vya Mhezi, Mteke na Mtunguja. Utekelezaji wa mradi huo utagharimu Sh. bilioni 1.3 hadi utakapokamilika.

Huo ni mradi wa tatu kujengwa na taasisi hiyo katika Wilaya ya Same na kuwezesha watu 6,350 kupata maji. "Nyie ni marafiki wazuri kwa kuwa mnashirikiana na serikali kujua vipaumbele vyetu na ni wawazi kwa kila mnachokifanya. Tunaendelea kuwakaribisha kuifanya Same kuwa ya tofauti," alisema Senyamule.

Pamoja na mambo mengine, mkuu huyo wa wilaya aliwashukuru wahandisi hao na Rotary Club kwa kuendelea kutoa fedha na kukubali kufadhili vijiji vingine vitatu miradi ya maji na huduma za afya. Wakati wakitoa utambulisho wao kwa Mkuu wa Wilaya, Mhandisi Steve Jones na Mhandisi Dave Millard kutoka Lowa Milard walisema wamefika Same kufuatilia maendeleo ya mradi wa maji unaojengwa katika kata ya Mhezi kwa ufadhili wa taasisi hiyo.

# Kesi tuhuma za wizi kunguruma Juni 25

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KESI ya madai ya wizi wa zaidi ya Sh. milioni 60 za wanafunzi wa kozi ya ualimu katika Chuo cha Ualimu Moshi inayowakabili watumishi wawili tofauti, itaanza kunguruma katika Mahakama ya Wilaya ya Hai Juni 25, mwaka huu.

Wanaokabiliwa na kesi hiyo ni aliyekuwa mhasibu wa chuo hicho, Sarafina Mbwambo, na Ofisa Masoko wa Chama cha Akiba cha Kuweka na Kukopa (Saccos) cha KKKT.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Hai, Devotha Msofe.

Shauri hilo lilikuwa lianze kusikilizwa juzi, lakini halikuendelea, baada maelezo yao kugundulika kuwa na dosari pamoja na wakili anayewatetea wadaiwa hao, kushindwa kufika mahakamani kwa madai kwamba alikuwa na kesi nyingine Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi.

Kesi hiyo namba 45 ya mwaka 2019, ilifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Februari 27 kwa wadaiwa hao kusomewa makosa mawili likiwamo la kughushi nyaraka za benki za malipo ya ada ya wanafunzi wa chuo hicho.

Wanadaiwa kwa pamoja kula njama na kujipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 60,230,000 kinyume cha kifungu cha 270 na kifungu kidogo cha 16 (i) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai cha Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.

Kabla ya mahakama kupanga tarehe ya kuanza kusikiliza kesi hiyo, mwendesha mashtaka wa serikali, Lobulu Mbise, alidai kuwa wadaiwa hao kwa pamoja mnamo Aprili 17, mwaka 2018, katika maeneo ya Moshi walikula njama za kughushi nyaraka za benki ya CRDB kupitia wakala wa benki hiyo.



ILO: Hawa ndio watumishi wa ndani, wanaishi hivi

Ukurasa 15




UCHUMI

## Huawei imeegeshwa hatarini kupoteza hadhi ya'simu janja'

Ukurasa 16

# BUFE

Ijumaa Juni 14, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Hoja sita 'zilizoshindikana' Bunge la Bajeti

Ukurasa 14

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Hoja sita 'zilizoshindikana

Na Sanula Athanas, Dodoma



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akiwasilisha mpango wa ukomo wa bajeti.

MAKADIRIO ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yaliwasilishwa bungeni jijini Dodoma jana jioni na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk.Philip Mpango.

Bajeti hiyo inalenga takriban shilingi trilioni 33, kwa mujibu wa Mpango wa Ukomo wa Bajeti, ambayo ni ya nne kuwasilishwa tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani Novemba 5, mwaka 2015.

Tangu kuanza Bunge la Bajeti, Aprili 2 mwaka huu, hoja ziliibuka wakati wa mijadala ya kisekta. Baadhi zilitolewa ufafanuzi na serikali na kuridhiwa na Bunge, zingine zililazimika kupelekwa kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya ufafanuzi wa kina.

Katika mijadala hiyo, uongozi wa Bunge ulilazimika kuzipeleka hoja za msingi sita mbele ya kamati hiyo, baada ya wabunge kushindwa kufikia muafaka na serikali wakati wa mijadala ya kisekta, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka ujao wa fedha.

Hoja zilizotua mbele ya kamati hiyo nyeti, ni pamoja na changamoto zilizojitokeza katika ugawaji vitambulisho vilivyoandaliwa na serikali kwa ajili ya wajasirimali na watoa huduma wadogo, pamoja na serikali kutoa taulo za kike bure kwa wanafunzi.

Pia, zilizojitokeza hoja za ombi la kuongeza makato ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli yanayouzwa, ili kutunisha mfuko wa maji; na kudorora ununuzi wa ngozi nchini.

Nyingine ni makandarasi watoa huduma na watumishi wa umma kutolipwa malimbikizo ya madai yao, sambamba na kupunguzwa kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa viwanda vya ndani.

Akizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Bunge mjini hapa mapema wiki hii, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, George Simbachawene, anasema walikuwa wanaendelea na majadiliano na serikali kuhusu hoja hizo, kabla ya makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, yaliyokwishwa wasilishwa jana.

**VITAMBULISHO WAJASIRIAMALI**

Wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha, wabunge wa pande zote mbili walieleza changamoto zilizojitokeza katika ugawaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali na watoa huduma wadogo.

Wabunge waliwalalamikia baadhi ya watendaji serikalini kwamba wanawakamata na kuwaweka ndani watu wajasiriamali, mfano hai ni mafundi ujenzi waliokutwa katika majukumu yao bila ya kuwa na vitambulisho hivyo.

Pia, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, ilihoji zinakoenda fedha zinazotokana na mauzo ya vitambulisho hivyo, kwa maana ya shilingi 20,000 kwa kila kitambulisho.

Wizara ya Fedha na Mipango, ilifafanua fedha hizo zinapelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali,

> **"Tusipoangalia, bidhaa zinazozalishwa nchini huenda vikashindwa hata kushindana na bidhaa zinazotoka nje. VAT ni somo gumu na pana, nchi kama Ufaransa wana utaratibu ambao bahati kwao ni 'very smart', lakini kwa nchi zetu hizi ni 'very complicated'.**

kama ilivyo kwa makusanyo mengine. Hata hivyo, kambi ya upinzani haikukubaliana na majibu hayo.

Katika kujadili suala hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ilidai serikali imekosea kuja na utaratibu huo kwa kuwa utaikosesha mapato mengi.

Ilitoa mfano wa mjasiriamali mdogo aliyekuwa analipa tozo ya soko shilingi 500 kila siku, lakini sasa analipa shilingi 20,000 kwa mwaka, badala ya shilingi 182,500 kwa kipindi hicho.

**MALIMBIKIZO MADENI**

Simbachawene anasema, hoja ya malimbikizo ya madeni kwa watumishi wa umma, makandarasi na watoa huduma, pia imefika mbele ya kamati yake na wanaendelea na majadiliano na serikali.

Wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya kisekta, wabunge waliitaka serikali kulipa malimbikizo ya mabilioni ya shilingi inayodaiwa na walimu, pia watumishi wengine wa umma, pamoj na makandarasi watoa huduma wanaodai kwa muda mrefu.

Mbali na watumishi wa umma, miongoni mwa watoa huduma wanaoidai serikali ni mawakala waliosambaza mbolea na pembejeo kwa wakulima. Serikali ilishaeleza kuwa inafanya uhakiki wa uhalali wa madai yao kabla haijaidhinisha malipo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, George Simbachawene. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# n’ Bunge la Bajeti



Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza jambo.

**TAULO ZA KIKE**

Mwaka jana serikali iliridhia ombi la wabunge kuondoa kodi kwenye taulo za kike, lakini imebainika kuwa licha ya uamuzi huo, bei ya bidhaa hiyo haijashuka.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inaendelea kujadiliana na serikali kuangalia uwezekano wa kuiingiza bidhaa hiyo katika mpango wa serikali wa kutoa elimu bila malipo ili wanafunzi wapatiwe taulo za kike bila malipo.

Mbunge wa Viti Maalum, Upendo Peneza (Chadema), aliwasilisha hoja hiyo bungeni mwaka jana, akieleza changamoto katika upatikanaji wa taulo za kike hasa vijijini, imechangia wasichana wengi kufanya vibaya katika masomo, kutokana na mahudhurio shuleni wanapokuwa kwenye siku zao.

**MAFUTA SH. 50**

Hoja ya kuongeza makato ya Sh. 50 kwa kila lita ya petroli na dizeli inayonuliwa, ilikuwa miongoni mwa hoja za msingi zilizotua kwenye Kamati ya Bajeti wakati wa mkutano wa Bunge la Bajeti mwaka jana.

Serikali ilikataa ombi hilo ikieleza kuwa uamuzi huo utasababisha mfumuko wa bei kwa kuwa mafuta yakipanda kutapaisha bei ya bidhaa nyingine.

Hata hivyo, hoja hiyo iliibuka tena mwaka huu wakati wa mkutano unaoendelea wa Bunge, watunga sheria wakiamini kuongeza makato hayo kutasaidia kutunisha Mfuko wa Maji na kutatua changamoto ya upatikanaji wa nishati hiyo nchini.

**UNUNUZI WA NGOZI**

Simbachawene, aliyewahi kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), anasema kamati yake inaendelea na majadiliano na serikali kuangalia namna ya kutatua changamoto iliyojitokeza katika soko la ngozi nchini mwaka huu.

Kiongozi huyo wa kamati, anasema uamuzi wa serikali wa kuja na utaratibu mpya wa udhibiti wa ngozi ya Tanzania, umekwamisha isinunuliwe nje ya nchi kwa ajili ya malighafi ya uzalishaji.

“Ngozi haiendi tena nje kwa ajili ya malighafi. Kuna watu siku hizi wamejitokeza wananunua ngozi kwa ajili ya kula. Serikali iliamini kwa kuja na utaratibu mpya wa kodi asilimia 80 ya soko, ingevisaidia viwanda vya ndani lakini matokeo yake viwanda vimeshindwa kununua ngozi,” alisema.

**VAT VIWANDANI**

Simbachawene, pia anasema kamati yake inaendelea na majadiliano na serikali kuangalia jinsi ya kuvisaidia viwanda vya ndani, kwa kupunguzia VAT kwenye bidhaa zake ili vishindane na viwanda vya nje.

“VAT kwenye viwanda vya ndani lazima tufanye jambo fulani kusaidia viwanda vyetu vya ndani, hasa vinavyotumia malighafi inayozalishwa nchini, mfano mazao ya kilimo.

“Tusipoangalia, bidhaa zinazozalishwa nchini huenda vikashindwa hata kushindana na bidhaa zinazotoka nje. VAT ni somo gumu na pana, nchi kama Ufaransa wana utaratibu ambao bahati kwao ni ‘very smart’, lakini kwa nchi zetu hizi ni ‘very complicated’.

“Unaweza kumpa mtu ahueni ya kodi hata kwa kumwondolea kabisa, lakini bado akaamua kuleta malighafi kutoka nje. Eneo hili kwa kweli ni shida na ndiyo shida ya umaskini,” Simbachawene anasema.




Utumikishaji watoto unasura nyingi, kulingana na mazingira. Pichani, baadhi ya watoto wakiwa katika biashara jijini Arusha. **PICHA:GETRUDE MPEZYA.**

## ILO: Hawa ndio watumishi wa ndani, wanaishi hivi

**Na Mwandishi Wetu**

NI kawaida katika maeneo mengi nchini na duniani, watoto kuajiriwa kwa ajili ya kutumikia shughuli za majumbani. Hawa wanaitwa watoto wa ndani.

Inadaiwa katika maisha ya ushirikiano kati ya waajiriwa na kada hiyo, watoto hao wanaonewa zaidi.

Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO), limetoa tafsiri katika hilo. Kupitia kitabu chake chenye maelezo mafupi, kiitwacho ‘Kazi za Ndani Zenye Madhara kwa Watoto’ ikifafanua;

“Utumikishwaji wa watoto wa kazi za ndani kwa kawada haijumuishi kazi ndogondogo zinazofanywa na wanafamilia.”

ILO inataja shughuli za kada hiyo katika maeneo ya mijini kuwa ni: “Zinajumuisha hasa kufanya usafi, kupika na kuwatunza watoto na wazee.

“Katika maeneo ya vijijini, kuna uwezekano wa watoto pia kuishiriki katika shughuli za kilimo. Baadhi ya shughuli za kawaida zinazowafanywa na watoto na wafanyakazi wa ndani,” inasema ILO.

Orodha iliyopo kwa mujibu wa shirika hili la kazi ni: Upishi; kusafisha jiko na vifaa vyake; kupokea wageni; kufua na kupiga pasi nguo, kushona; kusafisha na kupaka rangi viatu; kupanga chumba na kutandika vitanda; kusafishaji vitu vya samani; kufagia na kupiga deki sakafu, vyoo, bafu na maeneo ya nje; na kuosha vyombo vya usafiri.

Mengine katika orodha hiyo, inajumuisha: Kukarabati vifaaa na makazi; kutoa huduma na kusindikiza watu; kutunza na kuwasafisha wanyama wafugwao; kununua na kuhifadhi vitu vya nyumbani; kutafuta na kusomba maji; kutafuta na kubeba kuni na nishati nyinginezo na kutupa taka.

ILO kupitia maandiko yake inasema: “kuna uwezekano mkubwa wa watoto wafanyakazi wa ndani kuwa wengi wao ni wasichana, lakini kuna nchi chache ambako wavulana ni wengi.”

- **Hii ni kwa mujibu wa maandiko ya ILO.**

BIASHARA

KUTOKA MVUTANO KIMATAIFA...

# Huawei imeegeshwa hatarini kupoteza hadhi ya 'simu janja'

•Soko lake tegemezi limeachwa njia panda •Marekani imeibana, 'inapumulia' China

**Na Nimi Mweta**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Huawei ya China hivi sasa inatafuta njia za kuendesha biashara na kushindana na kampuni za Marekani, baada ya kampuni kubwa ya Google inayotamba katika mtandao wa kimataifa, intaneti kuiweka kando kwa amri ya utawala wa Rais Donald Trump.

Hatua hiyo iliwashtua watumiaji wa simu za Huawei kote duniani, lakini kwa uongozi wa kampuni hiyo haikuleta mshtuko mkubwa, ukisema ulikuwa unaandaa njia tofauti ya uendeshaji wa 'application' zake za mtandao. Kimsingi ilitaka ikwepe kutegemea kampuni ya Marekani.

Hata hivyo, hatua ya 'google' haitawahusu watumiaji waliopo sasa wa simu za Huawei, ingawa baadaye hawatakuwa na uwezo wa kuingiza 'applications' zinazotegemea mfumo wa Google.

Hayo ni baada ya Google kuondoa biashara na Huawei inayogusa mifumo ya kompyuta na simu, kutoa michoro ya utumiaji na huduma za kitaaluma kwa kampuni hiyo ya China.

**MPANGO MBADALA**

Taarifa kutoka Huawei inasema kuna 'mpango mbadala' endapo vikwazo vya Marekani vitahatarisha ushirikiano na Google, kuanzia wakati huo wadadisi wa masuala ya kompyuta wanatafuta Huawei itaenda vipi.

Baada ya hatua hiyo ya Google, inayotokana na vikwazo vya utawala wa Rais Donald Trump kupunguza nguvu za China kiuchumi na kuzuia kupanuka kwa vifaa vya China kama simu za Huawei kutamalaki zaidi katika soko la dunia, mipango ya kampuni hiyo ya simu inaingia katika kitendawili.

Dhana ya msingi inayoikabili ni kutoa mpango wa uendeshaji simu zake, kwa maana ya kampuni zingine za simu za mkononi zitakazotaka kutumia mfumo huo mpya, tarajiwa badala ya ule unaotegemea Google.

Hiyo ni kwa vile simu za China ni rahisi zaidi na inaweza kuwafikia wateja wa Google, bila ya kuitegemea kampuni hiyo ya Marekani kuwapa njia hiyo, kama katika mawasiliano mengine.

Katika eneo la ushindani, itakuwa mtihani mgumu kwa Huawei kupambana na kampuni ya Marekani. Ni matumizi ya mawasiliano ya ngazi ya kisasa zaidi aina ya 5G, ambayo ndio inaanza kusambaa duniani.

Ni aina inayoguswa na uwezo wake kuingia katika maeneo nyeti ya kiusalama ni mkubwa. Serikali ya Marekani inazitaka nchi zote zinazoshirikiana na Marekani katika masuala ya usalama kuondoa mwingiliano na Huawei, la sivyo Marekani itakata ushirikiano huo.

Kuna nchi tayari zimeshachukua hatua kutimiza masharti hayo na nyinginezo zinakamilisha uzuiaji wa mwingiliano wa kimtandao na Huawei.

***MTIHANI WA LESENI***

Uwezekano wa kampuni hiyo kutumia leseni huria za mifumo ya uendeshaji mawasiliano ya kompyuta na simu bila hatimiliki maalum kuwafikia wateja ambao kimsingi wanajumuika katika mtandao wa Google, pia uko shakani.

Leseni hizo zina kampuni ambayo moja ya wateja wake wakubwa ni Google, hasa kwa matumizi ya 'applications' muhimu kama Gmail na YouTube, zinazohitaji mkataba na Google na hazifikiwi tu kwa kutumia leseni huria.

Matokeo yake ni kuwa simu za Huawei ziko hatarini kuwa siku za kutumia nchini China, ambako kampuni inashikilia takriban asilimia 92 ya soko la simu na hali hiyo ni maeneo yanayogonganisha China na Marekani, kuwa kuna mfumo wa kuilinda Huawei katika soko la China. Ila tatizo kubwa zaidi ni mahusiano kati ya Huawei na serikali ya China, kwani mwanzilishi wake Ren Zhengfei ni ofisa wa zamani wa Jeshi la Ukombozi la Watu wa China.

Tatizo la kuwekewa vikwazo na Marekani, inabeba sura pana si kwa kampuni za Marekani pekee yanayotakiwa kutimiza masharti ya vikwazo, bali kampuni yoyote duniani yenye dhamira ya kufanya biashara na kampuni ya Kimarekani.

Ni mbinu inayogusa njia ya kuingia katika mitandao, siyo rahisi kufikia mfumo wa Google bila ya kuwa na mikataba, hivyo itabidi Huawei ihamishie operesheni zake kwa nchi tofauti iwe na mkataba nayo.

Hata hivyo, nchi za ukanda wa mashariki ya mbali ni washirika wa karibu wa Marekani, hivyo bado si ukanda mzuri wa Huawei kujipanga.

Wachunguzi wa habari wanasema wataalamu katika kampuni ya Huawei bado walikuwa wanatafuta athari za kuondolewa kuingiliana na Google, huku wataalamu wa mifumo ya 'microchip' inayotumika kuunda kompyuta na simu wakisema wazi haitakuwa rahisi kwa Huawei kustahimili kishindo hicho.

Maofisa wa juu wa Huawei walikuwa wanasisitiza kampuni ya teknolojia ya Android (inayotumika kuunganisha mifumo ya simu, mawasiliano kwa leseni) hawana haki kisheria kuwazuia wanaotumia leseni huria (bila hatimiliki ya mifumo husika) kuingiliana na wenye leseni hizo huru.

Hata hivyo, kunaweza kuonekana kama kuvunja vikwazo vya Marekani kwa kampuni hizo. Hiyo inabeba maana kwamba, simu za Huawei ambazo ziko sokoni au zinatumika, ndiyo zitakazokuwa na uwezo wa kuingia mtandao wa Google, ambao kimsingi ni lazima kwa kila mtumiaji wa 'simu janja.'

***UWANJA WA CHINA***

Ila kwa upande wa soko la China ambako mifumo ya uendeshaji sekta ya mawasiliano una vizuizi kadhaa, Huawei itaendelea kutamalaki soko la China, kwa kukusanya mifumo ya taarifa za vyanzo huru hata kama zina uhusiano na maeneo ambayo Google ina maslahi.

Hata hivyo, itakuwa katika wakati mgumu kufanya hivyo nchi za nje, hivyo soko la simu zake mpya litakuwa China. Kimsingi, nje ya matumizi ya 'Gmail' na 'YouTube.' Mengine huwa hayahitaji mikataba ya moja kwa moja na 'Google' ila wasambazaji wa karibu.

Wachunguzi wa habari wanasema kuwa, hatua hiyo haitakuwa na athari katika soko la China, kwa sababu mifumo na 'application' za Google zimepigwa marufuku nchini humo.

Hiyo inaiacha Huawei na washirika wake wawili, Tencent na Baidu, umiliki wa soko. Vivyo hivyo, Huawei ina mtandao mpana wa kuuza simu kote duniani, lakini barani Ulaya 'litapauka' kwani inatumia 'application' kadhaa kwa leseni kutoka Google, na 'application' hizo zikikosekana, ni wazi simu za Huawei hazitakuwa 'simu janja' kama nyingine.

Inaelezwa kwamba, hata kama Huawei ingezindua mfumo mwingine wa 'simu janja,' haitaweza kukwepa wateja wa Google, katika kufanikiwa kimataifa au kuwafikia wateja wa Google kwa njia hiyo mbadala.

***MZOZO ULIPOANZIA***

Mzozo kuhusu Huawei, ulianza mwishoni mwa mwaka 2017 wakati Baraza la Usalama wa Taifa nchini Marekani, ulipoiweka kampuni hiyo kama moja ya asasi hatarishi za kibiashara zenye uwezo wa kugusa mifumo ya kiusalama.

Hiyo ilitokana na kampuni kuanza kusambazwa simu za viwango vya kisasa vya 5G zenye uwezo mkubwa kukusanya vyanzo vya utumiaji na ukusanyaji habari, huku uhusiano wa kampuni ya Huawei na serikali ya China ukiifanya kuwa tishio la kiusalama kwa Marekani.

Huawei ilikuwa inakuwa kwa kasi katika udhibiti wa soko duniani, nyuma ya vigogo Samsung ya Korea Kusini, hasa eneo la mauzo kimataifa.

Hitilafu hiyo mpya kuhusu Huawei inatoa changamoto ya ziada kwa serikali ya Rais Xi Jinping, katika kufuatilia mpango wa 'Belt and Road,' uliopania kuunganisha mabara yote duniani kibiashara kutoka vianzio vya kinachoitwa 'majiji ya masoko makubwa duniani ya China.'

Utekelezaji wa mpango huo, kimsingi umepiga hatua kubwa kuanzia Asia ya Mbali, Kati na Ulaya Magharibi.

Ila unaweza kuvurugwa endapo kampuni ya China itaendelea kuwekewa vikwazo na Marekani, halafu nchi za Ulaya zilazimike kutekeleza vikwazo hivyo, labda isifanye biashara na kampuni ya Marekani.

Hiyo ina maana kwamba, itabidi Huawei iuze hisa wapate washirika kutoka nje watakaohakikisha kinachoelewa 'haina uhusiano wa karibu' na mifumo ya kijeshi na kiusalama ya China katika kuendesha ushindani halisi nchini.

Pia kunaelezwa hivi sasa ni matokeo ya sera za China, utandawazi nje na uzalendo kwa ndani.

> **Katika eneo la ushindani, itakuwa mtihani mgumu kwa Huawei kupambana na kampuni ya Marekani. Ni matumizi ya mawasiliano ya ngazi ya kisasa zaidi aina ya 5G, ambayo ndio inaanza kusambaa duniani.**




Rais Donald Trump, akitoa tamko kuhusu simu za Huawei. Picha nyingine ni aina hiyo ya simu. **PICHA: MAKTABA.**




## BIASHARA KATIKA PICHA



Wauza mboga wakiendelea na biashara yao eneo la Goba, jijini Dar es Salaam. Wataalamu wa lishe huwa wanashauri mboga zisikae juani kwa muda mrefu kwa vile zinaweza kupoteza viinilishe.



Vijana wa Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, ambao wako kwenye majukwaa ya vijana wanaojishughulisha na biashara mbalimbali wakiwa kwenye semina ya ujasiriamali. PICHA ZOTE: SABATO KASIKA



Wachuuzi wa viazi wakisubiri wateja katika Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam. **PICHA:MIRAJI MSALA**

UCHUMI



Sehemu ya shamba ambalo limeandaliwa tayari kwa ajili ya kilimo. Ardhi bora na matumizi yake, ni sehemu ya mafanikio katika kilimo, kama kinachofanyika mkoani Morogoro. **PICHA: MAKTABA.**

# Kilimo cha kisasa kinavyowapandisha hadhi 'vya kunufaika' wakulima Moro

- Aliyeambulia debe 4, sasa ni wa gunia 5
- Misitu inayoteketea nayo imebaki salama

**Na Christina Haule, MOROGORO**

BADO ukweli unaendelea kusimama. Kilimo cha kisasa kina maana kubwa, si kwa kumlisha mlimaji pekee, bali sura pana ya ajira, biashara na uwekezaji, hifadhi ya mazingira.

Ujumla wake hatua katika sura ya uchumi wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla. Kimsingi, inarejea tafsiri, 'Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa.'

Ndivyo inavyotafsiriwa, kwa maana inashika sura ya nchi na maisha binafsi katika awamu zote za uongozi wa nchi, tangu kupatikana uhuru mwaka 1961.

KILICHOKO MOROGORO

Mtazamo huo katika kushuka ngazi ya chini, hivi sasa mkoani Morogoro kuna kilimo kinachoendeshwa kupitia inayotambuliwa kuwa 'Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS)', maarufu kama mkaa endelevu.

Ni mradi ambao umewanufaisha wakulima wa vijiji 30 vinavyotekeleza mradi huo, kikiwamo Matuli kilichopo katika kata ya Ngerengere, wilayani Morogoro.

Hiyo inaelezwa ni kutokana na kuongeza uzalishaji wa mazao, huku wakihifadhi misitu na kufikia malengo waliyokusudia.

Mkulima Prisca Mkude, anasema amelima eneo la robo ekari iliyompatia gunia tano, wenzake waliopakana mashamba walikosa kabisa.

Pia, anarejea zamani alivyokuwa akipata plastiki nne hadi gunia moja tu katika kilimo ndani ya eneo hilo hilo tajwa. Anarejea njia mojawapo wanayotumia katika kilimo cha kisasa, ni kuweka majani wanayolima shambani, ili kupata mbolea na kurutubisha ardhi hiyo anayolima.

Katika hilo, Prisca anasema kinachofanyika ni kuchimba mashimo marefu, wanahifadhi maji kwenye shina la mmea. Matunda yake anakiri kuwasaidia kupata mbolea ya kupandia na kukuzia.

Anasema, kabla ya mradi walihama eneo la kilimo na pindi wanapokosa mazao na kuhisi udongo umeisha nguvu, wakulima hao walikataa na kuchoma misitu kwa ajili ya kilimo katika eneo jingine jipya.

**WATAALAMU KILIMO**

Ofisa Kilimo kata ya Matuli, Maleko Dangaya anasema, kupitia kilimo hifadhi, wameweza kupata mabwana shamba 27 na wakulima 270 waliopata mafunzo ya mbinu bora za kilimo, kulingana na mabadiliko ya tabia nchi.

Ofisa huyo anawataja maadui wa misitu wapo wawili, kuwa ni uchomaji mkaa na uandaaji mshamba kwa kufyeka msitu.

Hivyo, anakiri kwamba mafunzo ya kilimo hifadhi kinachoendana na hifadhi ya mazingira na utunzaji misitu umemletea manufaa makubwa katika kilimo.

Dangaya anasema, tangu mradi uanze mwaka 2016, mpaka sasa wana mashamba darasa tisa yenye jumla ya wakulima 270 waliojifunza kupitia mradi wa mkaa endelevu.

> **"Ofisa wa Kujenga Uwezo wa mradi huo, Simon Lugazo, hekta 469 za misitu, hasa aina ya miombo inapotea kila mwaka, kutokana na kilimo na uzalishaji mkaa holela.**

Pia, anasema suala la moto kuvamia misitu, linachangiwa kwa kiasi kikubwa na uandaaji mashamba, huku moja ya kanuni za kilimo bora ikutaja mwiko wa kuandaa mashamba kwa kuchoma moto msitu.

Charles Leonard, Meneja Mradi wa TTCS, anasema shughuli za kilimo zinaongoza kwa uharibifu na ufyekaji misitu nchini, ikikadiriwa asilimia 89 ya uharibifu unasababishwa na kilimo hasa cha kuhamahama.

Pia, meneja huyo anasema imeshapoteza hekta 469 za misitu nchini katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2017.

Leonard anasema, mradi huo unaendeshwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ushirikiano na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), pia Taasisi ya Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO), kupitia Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa.

Ni kazi inayofanyika kwa kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC) kupitia kitengo cha Kilimo Hifadhi nchini, wamewafundisha wananchi kilimo chenye tija, kinachoongeza kipato, kupitia shamba lile lile, pasipo kuhama.

**MASHAMBA MAALUM**

Leonard anasema, hadi ndani ya vijiji 30 wana mashamba darasa katika kila kijiji na mradi na wanawezesha kuendesha kilimo cha hifadhi.

Anasema, wakulima wanafanywa marafiki wa mazingira kwa kuendelea ardhi kuwa na rutuba, huku uzalishaji noa ukiongezeka.

Emmanuel Lyimo, Mkurugenzi Msaidizi wa TFCG, anasema kupitia mradi huo, wamefanya utafiti katika maeneo 120 nchini yenye uharibifu mkubwa wa misitu na kubaini yameharibika kwa asilimia 89, kutokana na kilimo cha kufyeka misitu.

Anasema, zao kubwa walilolima kulikofyekwa msitu ni mahindi na asilimia 36 ya eneo hilo linatumiwa na wakataji mkaa holela, huku kilimo kikishika kasi kwa usafishaji kupitia uchomaji misitu na ukataji miti ovyo.

Lyimo anasema, kupitia mradi wao wameona haja ya kilimo hifadhi, wakizingatia kwamba wanavijiji wanatambua thamani ya miliki ya misitu ya vijiji vyao.

Ushauri wake ni kwamba, watengeneza sera watambue umuhimu wa wanavijiji, ili sera zinapotengenezwa izingatie pamoja na rasilimali zao mhali waliko, ikijumuisha misitu inayopaswa kutunzwa na wakati huohuo inasaidia upatikana wa maji.

Lyimo anasema, usimamizi thabiti na biashara endelevu ya mazao ya misitu kuingizwa katika maisha ya jamii, inapaswa kuwa endelevu, ili iwanufaishe katika misitu yao, wakishirikiana na serikali za vijiji, kwa maendeleo ya moja kwa moja kiuchumi kupitia zao la misitu.

Ofisa Maliasili wa Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa, anashauri mfumo huo wa kilimo ufanyike katika maeneo yote nchini, kwani umeonekana kuwa bora nchini kwa kiasi kikubwa.

Ofisa wa Kujenga Uwezo wa mradi huo, Simon Lugazo, hekta 469 za misitu, hasa aina ya miombo inapotea kila mwaka, kutokana na kilimo na uzalishaji mkaa holela.

Lugazo anasema, asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini kote nayo inatokana na mkaa, hasa ya miti ya miombo, kwa kiwango cha asilimia 97 nchini.

Anasema mradi wa mkaa endelevu, una mpango wa kuendelea kutoa elimu kwa wakulima, wasaidie uhifadhi wa misitu, ili kuimarisha na kuleta tija ya kilimo, wakiondokana na mtindo wa kuhamahama.

UCHUMI



Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) katika ziara ya bodi hiyo, mwaka jana katika Bandari ya Kasanga, mkoani Rukwa. Kutoka kushoto ni Renatus Mkinga, Jayne Nyimbo na Aziz Kilonge. Kulia ni Kaimu Meneja wa Bandari ya Kigoma, Ajuaye Msese. **PICHA: MTANDAO**

MENEJA TPA MWANZA:

# Tunajiinua ziwani kwa kuzipa uhai bandari bubu, mapato kwa Tehama

- Meli mbovu, malori yamewashusha
- Wanawafuata wateja waliojiengua

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), inamiliki na kusimamia bandari kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na bandari ndogo za Kilwa, Lindi, Mafia, Pangani na Bagamoyo zilizoko mwambao wa Bahari ya Hindi.

Zaidi ya hapo, TPA pia inamiliki bandari kadhaa katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa; Ndani ya Ziwa Victoria zinapatikana bandari kuu za Mwanza, Bukoba, Kemondo Bay (mkoani Kagera) na Musoma.

Katika Ziwa Tanganyika, kuna bandari za Kigoma na Kasanga na Ziwa Nyasa ni Mbamba Bay (Wilaya ya Nyasa) na Itungi (Kyela).

Katika kuhakikisha bandari hizo zinafanya kazi kikamilifu, TPA iko katika mradi wa kujenga inayotekeleza miradi ya ujenzi wa gati mpya za kisasa, kukarabati za zamani na kujenga bandari mpya, katika maeneo ambako kulikuwa 'bandari bubu.'

**ZIWANI VICTORIA**

Waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari wanatumia siku sita kutembelea bandari kuu za Ziwa Victoria ambazo ni Mwanza, Bukoba, Kemondo Bay na Musoma.

Nipashe ni sehemu ya timu ya wanahabari waliozuru Ziwa Victoria na kutembelea bandari ndogo katika mwambao wa ziwa. Hapo inajumuisha bandari za Maisome, Kome, Bukondo, Kahunda, Nkome, Miharaba, Buchesi, Solima na Karumo, Ntama, Kanyala au Lushamba zilizopo mkoani Mwanza.

Nyingine ni Chato na Nyamirembe za mkoani Geita; Kyamkwikwi na Magarini mkoani Kagera na Shirati na Kinesi mkoa wa Mara.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, ambaye ndiye mwenyeji wa safari hiyo, katika taarifa yake ya miradi inayoendelea bandarini hapo, anasema TPA ilianzishwa kisheria mwaka 2004 na ilianza kazi mwaka 2006, ikirithi majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Anasema TPA, ina majukumu ya kumiliki na kuendeleza bandari zilizoendeshwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) katika Maziwa Makuu, hivi sasa ikiwa na maono ya kuongoza katika biashara ya bandari na utoaji huduma ya uhakika katika mtandao wa uchukuzi katika kanda hiyo.

> **Kaimu Meneja wa Bandari ya Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, ambaye ndiye mwenyeji wa safari hiyo, katika taarifa yake ya miradi inayoendelea bandarini hapo, anasema TPA ilianzishwa kisheria mwaka 2004 na ilianza kazi mwaka 2006, ikirithi majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania.**

"Azma ya TPA ni kuendeleza na kusimamia bandari ziweze kutoa huduma zenye uhakika, bora, nafuu na zenye maslahi kibandari kwa kutumia mbinu na teknolojia ya kisasa katika ukanda wa mashariki, kati na kusini mwa Afrika," anasema Lwesya.

Anafafanua kuwa, mbali na bandari wanazohudumia, kuna baadhi wameshaanza kuziendeleza kwa kuzijengea miundombinu katika miradi ya kuifanya bandari ndogo, akizitaja kuwa ni Ntama, Lushamba na Kyamkwikwi.

"Pia katika mwaka huu wa fedha kuna bandari ambazo zimepangiwa miradi ya uendelezaji wa miundombinu," anasema Lwesya, nazo akiziorodhesha kuwa ni

INAENDELEA UK.20



Kaimu Meneja wa Bandari ya Mwanza, katika Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, akionyesha meli ya mizigo inayobeba mabehewa ya treni kutoka Ziwa Victoria kwenda nchini Uganda. **PICHA: MARY GEOFREY**

UCHUMI



Sehemu ya Bandari ya Bukoba katika Ziwa Victoria. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Tunajiinua ziwani kwa kuzipa uhai bandari bubu, mapato kwa Tehama

**INATOKA UK.19**

bandari za Nyamirembe, Magarini na Kasenda.

Lwesya anasema mtazamo ulioko ni kwamba zitahudumia mizigo na abiria na kwa sasa hakuna bandari inayohudumia makasha.

Anasema, kwa sasa kuna kituo kinasimamia bandari kavu za Fela iliyopo wilayani Misungwi mkoa wa Mwanza na Isaka, iliyopo wilayani Kahama, Shinyanga.

Kuhusu Bandari ya Mwanza, anasema zina miundombinu kongwe za kurithi, ikiwa na vifaa vya kisasa vya kuhudumia mizigo na abiria.

Anaitaja miundombinu hiyo, ni pamoja na magati, ghala la kuhifadhi mizigo, majanga ya abiria, daraja la kuunganisha reli, meli na chelezo moja kwa ajili ya matengenezo ya meli.

**UTENDAJI KAZI**

Lwesya anasema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kati ya mwaka wa fedha 2013/14 hadi 2017/18 shehena iliyohudumiwa katika Bandari za Mwanza ilikishuka kwa wastani wa asilimia 20.7.

Kwa mujibu wa Lwesya, hiyo ni kutoka tani 213,311 ya mwaka 2013/14 hadi tani 84,615.178 mwaka 2017/18 (Julai hadi Mei) shehena iliongezeka kwa tani 146,287.

Anataja sababu za kushuka shehena hizo ni kuchechemea kwa ufanisi wa huduma ya reli ya kati, iliyokuwa ikisafirisha shehena kubwa zinazoingia katika Bandari ya Dar es Salaam, kutoka nchi nyinginezo.

Lwesya anataja sababu nyingine ni kuharibika meli ya kampuni ya MSCL, zilizokuwa zinafanya safari zake katika ziwa hilo kwa upande wa Tanzania na nchini Uganda.

Pia, anataja ushindani wa kibiashara uliopo kati ya usafiri wa majini na njia ya barabara na kuwapo kwa ushindani kutoka bandari za watu binafsi.

Kuhusu idadi ya abiria, anasema katika kipindi cha miaka mitano imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka kwa wastani wa asilimia 19.8 na kwa mujibu wa Lwesya, imepungua kutoka abiria 593,281 mwaka 2013/14 hadi abiria 246,462 mwaka 2017/18.

"Mwaka 2018/19 idadi ya abiria ilianza kuongezeka baada ya ukarabati wa meli ya abiria ya MV Clarias. Pia, kuwapo meli za mwendo kasi za abiria MV Blue Bird na Mv Rafiki, ambazo safari zao zote ni kati ya Mwanza Kusini na Nansio Ukerewe," anasema Lwesya.

**ABIRIA KUPUNGUA**

Ofisa huyo wa TPA, anasema sababu za kupungua idadi ya abiria, ni ubovu wa meli ya MV Victoria, iliyoko katika matengenezo.

Meli hiyo, pamoja na Serengeti na Clarias, ni tegemeo kubwa la kusafirisha abiria katika Ziwa Victoria.

Anataja sababu nyingine ni ushindani katika njia ya barabara ambazo kwa sasa zinatumika zaidi na kuwapo kwa bandari binafsi na kwa upande mwingine kuongezeka safari za ndege za abiria kwenda na kutoka Bukoba.

Lwesya anaeleza kuwa katika meli zilizohudumiwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita katika maeneo hayo, zimepungua kwa wastani wa asilimia 33.4.

Anasema katika mwaka wa fedha 2013/14, idadi ya meli zilikuwa 2,682 na zilipungua na kufika meli 530 kwa mwaka wa fedha 2017/18. Katika mwaka wa fedha 2018/19, zilianza kuongezeka tena.

**ONGEZEKO MAPATO**

Anasema mapato yatokanayo na shughuli za kupakia na kupakua shehena bandarini yameongezeka kwa wastani wa asilimia 54.6 mwaka wa fedha 2018/19; kati ya

Julai hadi Aprili TPA imeingiza shilingi bilioni 1.138 ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Lwesya anataja sababu ya ongezeko hilo ni kufunguka tena njia ya Mwanza hadi Bandari ya Uganda na matumizi ya tozo linganifu tangu mwaka 2018, chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Anataja mchango mwingine ni wa maboresho katika kurejesha usafirishaji mizigo ndani bandarini Musoma na matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ukusanyaji mapato.

Maboresho hayo ya Tehama, anataja kutumika katika bandari za Kemondo na Mwaloni, Kyamkwikwi, Mwanza Kaskazini na Kusini, Isaka, Mwigobero Bukoba na Mwalo wake na Nansio.

Anasema, kurejea kwa wateja waliokuwa wameacha kutumia Bandari ya Mwanza Kaskazini na Musoma, pia maboresho ya shughuli za usafirishaji katika mashirika ya Shirika la Reli (TRC) na MSCL mchango wake.

Lwesya anasema, mikakati waliyo nayo bandarini ni kuwadumisha wateja wao wa kila siku, huku wakitafuta wateja wapya, kurudisha waliojiengua kutokana na sababu mbalimbali.

Aidha, mkakati unapiga hatua zaidi ya kuwarejesha walioondoka sokoni kutokana na sababu mbalimbali, ili kukuza wigo wa soko la wateja wao.



Bandari ya Itungi, iliyoko Kyela, mkoani Mbeya. **PICHA: MTANDAO**



# Afrika yaongoza utumikishaji watoto

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

BARA la Afrika limetajwa kuwa ndilo linaloongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wanaotumikishwa kwenye ajira mbalimbali za uzalishaji mali zikiwamo shughuli hatarishi za mashambani na kwenye migodi.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Utumikishwaji wa Watoto Duniani na Meneja wa kupinga utumikishwaji wa watoto kwenye mashamba ya tumbaku ujulikanao kwa jina la Prosper Umoja, Christopher Ruyenga.

Mradi huo unatekelezwa na Asasi ya Kiraia ya Winrock International chini ya ufadhili wa Shirika la Eliminating Child Labor in Tobacco Growing Program Foundation (ECCT) na unatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Tabora na Songwe ambayo ndiyo inayozalisha tumbaku hapa nchini.

Ruyenga alisema utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani (ILO), unaonyesha kuwa watoto milioni 218 wenye umri kati ya miaka mitano hadi 17 duniani wanatumikishwa na milioni 72.1 wanatumikishwa barani Afrika.

Alisema bara linalofuata kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto ni bara ya Asia na Pasifiki yenye watoto milioni 62.1, huku eneo lenye idadi ndogo ya watoto hao ikiwa ni nchi za Uarabuni lenye watoto milioni 1.2.

Alisema utafiti huo unaonyesha kuwa watoto wanaotumikishwa nchini Tanzania ni milioni 4.2 idadi ambayo alidai ni kubwa na inahatarisha ustawi wa watoto na kwamba utumikishwaji huo unawanyima watoto haki zao. "Katika Wilaya ya Chunya tumekuwa tukishirikiana na kampuni ya ununuzi wa tumbaku kupinga utumikishwaji huo na mpaka sasa tumewasaidia watoto 180 wanaoishi kwenye mazingira magumu kupata vifaa vya shule ili kuwaepusha na ajira za ututoni," alisema Ruyenga.

Alisema mbali na kuwasaidia watoto hao pia wametoa elimu ya ujasiriamali na vikoba kwa wanawake 180 ili wajiongezee kipato na kuepuka kuwatumikisha watoto. Baadhi ya wawakilishi wa kampuni ya ununuzi wa tumbaku katika mikoa ya Mbeya, Tabora na Songwe, walisema mbali na ushirikiano wanaotoa kwa serikali kukomesha utumikishwaji wa watoto, wameamua kutonunua tumbaku kwa mtu yeyote atakayebainika kuwa ameajiri watoto.

Mwakilishi wa Kampuni ya ununuzi wa tumbaku ya TLTC, Fabian Kababi, alisema kampuni hiyo ina programu maalumu ya kuwaelimisha wakulima kuhusu kutowatumikisha watoto mashambani na badala yake kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Alisema wanapita mashambani kutoa elimu hiyo na kwamba kwa sasa wakulima wameanza kuelewa na kuacha tabia hiyo ya kuajiri watoto kwenye mashamba.

"Wakulima wameanza kuelewa elimu tunayotoa maana maofisa kilimo wakitembelea mashambani, wakulima walioajiri watoto wanaanza kukimbia na hapo sisi tunaanza kuelewa kuwa wanaelewa elimu tunayotoa," alisema Kababi.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo yaliyofanyika katika Kata ya Lupatingatinga, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliwataka wakulima na wachimbaji wa madini kuacha kuajiri watoto na kwamba yeyote atakayepatikana atachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema yeye kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa wilaya hiyo, hatakuwa tayari wilaya yake kuwa miongoni mwa maeneo yanayoajiri watoto na watoto wote wanatakiwa wasome shule na kupata haki zao zingine za msingi ikiwamo kucheza.



Mwendesha baiskeli akiwa ameisheheni mzigo katika Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Waomba sera kumlinda mwanamke kwenye kilimo

**NA Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imeshauriwa kuandaa sera itakayomlinda mwanamke anayeshiriki kwenye shughuli za kilimo, kunufaika na rasilimali zilizopo na kujikwamua kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi katika jamii.

Ushauri huo ulitolewa jana na mwezeshaji mafunzo ya uongozi shirikishi, jinsia na demokrasia kutoka Shirika lisilokuwa la kiserikali la TGNP - Mtandao, Rehema Mwateba, ambayo yaliyowahusisha wazee wa mila, vituo vya taarifa na maarifa.

Alisema kuundwa kwa sera itakayomlinda mwanamke anayejishughulisha na kilimo itamsaidia kufurahia maisha, lakini kupata fedha ambazo zitamsaidia kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Alisema wanawake hasa waishio vijijini wengi hawahusishwi na wenzi wao kupanga matumizi msimu wa mavuno na wanapendekeza kuwapo na sera itakayomlinda mwanamke ili kupata haki ya kufanya maamuzi katika mavuno hayo.

"Tunahitaji sasa sera ya kutuongoza kuhakikisha wanawake wanapewa nafasi ya kufanya maamuzi ndani ya familia pindi msimu wa mavuno unapowadia ikilinganishwa na ilivyo sasa, wanaume wengi, huku Mbeya Vijijini ni wababe hawashiriki wenzi wao matokeo yake hutafuta," michepuko alisema Rehema.

Alisema unyanyasaji wa kiuchumi hasa msimu wa mavuno hurudisha nyuma jitihada za mwanamke kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa sababu ya kukosa fedha na kukatishiwa na waume zao.

Aliongeza kuwa kampeni ya 50 kwa 50 ambayo inapigiwa kelele na wadau mbalimbali lazima ianzie ngazi ya chini ambako kuna mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa na sio udiwani na ubunge peke yake kwa sababu wanawake wengi hawajiamini kugombea kutokana na kukosa fedha na ikizingatiwa wengi ni wakulima, lakini wanapovuna mazao wanakuwa hawana maamuzi.

Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa katika Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, alisema wanawake na wanaume wana haki ya kumiliki rasilimali zao kwa usawa bila ubaguzi wa aina yoyote kwa kisingizio cha jinsia.

Naye Kiongozi wa kimila kutoka kabila la Wasafwa, Aron Mwazyunga, alisema hatua ya kuwashirikisha viongozi wa jadi kwenye mafunzo hayo usawa na jinsia, kutasaidia kuongeza idadi ya wanawake kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa wao wanaushawishi mkubwa katika jamii.

# Mpango wa damu salama waomba wachangiaji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MPANGO wa Taifa wa Damu Salama, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, umeviomba vyombo vya ulinzi na usalama vya Mkoa wa Mbeya, taasisi za serikali na binafsi kujitokeza kuchangia damu ili Benki ya Damu Salama iwe na akiba ya kujitosheleza.


Hayo yalisemwa jana na Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Charton Meena, wakati akizungumza na Nipashe alieleza kuwa kumekuwa na uhaba wa damu kwenye hospitali mbalimbali kwa sababu ya mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia damu.

Alisema katika kuhakikisha kuna akiba ya kutosha kwenye benki za damu, wadau mbalimbali ikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama wanapaswa kujitokeza kuchangia damu ili kunusuru maisha ya wagonjwa.

Aidha, Meena aliwashauri wachangiaji damu wanaoamini kuwa kuchangia damu mara kwa mara kunasababisha damu kuisha haraka mwilini, badala yake alisema kuchangia damu husaidia kupunguza magonjwa mbalimbali ukiwamo ugonjwa wa kansa.

"Tumekuwa tukiwashirikisha wadau mbalimbali kuchangia damu hususani wanafunzi wa shule za sekondari, vyuo mbalimbali, lakini mwitikio wa vyombo vya ulinzi na usalama umekuwa mdogo pamoja na taasisi za serikali na binafsi hali inayosababisha kuwa na changamoto ya damu katika benki na kuhatarisha maisha ya wagonjwa," alisema Meena.

Alidai kuwa Kituo cha Uchangiaji Damu Salama cha Nyanda za Juu Kusini ambacho kipo katika Hospitali ya Wazazi Mmeta, kinategemewa kwa kiasi kikubwa kuhudumia mikoa yote minane kusambaza damu, hivyo ni jukumu la kila Mtanzania aliyekuwa na sifa ya kuchangia damu kujitokeza ili kunusuru maisha ya wagonjwa hususani wajawazito.





# Vituo vya afya 352 kupata vifaa vya kisasa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

IDARA ya Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imeagizwa kuweka vifaa vya kisasa kikiwamo cha upasuaji ambacho kinazuia utokwaji wa damu, kwenye vituo vya afya 352 vilivyojengwa na kukarabatiwa nchini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Selemani Jafo, baada ya kupokea vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 142 kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma ya afya vya Murugwaza na Nyamiaga mkoani Kagera ambavyo vimetolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamaji (IOM). Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Waziri Jafo alisema vifaa hivyo ni vizuri na vya kisasa vinaweza kufanya upasuaji wa aina hiyo na hata kwa mtu ambaye ana upungufu wa damu.

"Hii mashine ni nzuri na ya kisasa ambayo daktari anaweza kufanya upasuaji hata kwa mama mjamzito mwenye damu chache kwa sababu inauwezo wa kuzuia utokwaji wa damu wakati wa upasuaji, wote tunajua kuwa suala la damu kwa mama wajawazito ni tatizo, na hata upatikanaji wa damu kwa wakati ni shida," alisema.

Alisema kukiwa na kifaa hicho badala ya daktari kuhangaika kutafuta kumwongezea damu mama mjamzito ndipo amfanye upasuaji, lakini anaweza kumfanyia hata mwenye damu 5.

Waziri huyo alisema kwa sasa wakati ukamilishaji wa vituo hivyo ukiendelea na wameanza kujenga hospitali za wilaya 67 na hospitali mpya 27 ni vyema kuwa na vifaa ambavyo vitawezesha wananchi kupata huduma bora.

"Niagize idara ya afya ya ofisi yangu tukiwa tunaenda kwenye hatua ya kununua vifaa tuangalie aina hii ya vifaa tununue, hii mashine inauzwa kati ya Sh. milioni 3 hadi 4, wakati kifaa ambacho kinaweza kumsaidia daktari kupata mwanga wakati wa upasuaji hata kama hakuna nishati kinauzwa kati ya Sh. 600,000," alisema.

Naye Mwakilishi Mkazi wa IOM, Dk. Qasim Sufi, alisema shirika hilo limekuwa likishughulikia kuwalinda wahamaji ikiwa ni pamoja na kuwarejesha nyumbani wakimbizi.

Alisema waliamua kusaidia vifaa hivyo kutokana na hali waliyoiona wakati wakiwa kwenye operesheni ya kuwarejesha nyumbani wakimbizi wa Burundi.

Alieleza kuwa kulitokea ajali ambayo ilisababisha vifo vya watu 8, na majeruhi wengi waliweza kuokolewa kwa kupatia matibabu kwenye vituo hivyo, lakini walikutana na changamoto ya vifaa.

"Mimi mwenyewe niliingia kusaidia katika kuokoa maisha ya watu, ni tukio ambalo bado nalikumbuka, na sisi IOM bado tunaendelea na majukumu yetu na lolote linaweza kutokea huko, hivyo tukaona tusaidie hospitali hizi mbili vifaa mbalimbali ikiwamo hiki cha upasuaji ambacho kinaweza kumfanya mgonjwa asivuje damu nyingi," alisema.



Dereva wa Bohari ya Dawa (MSD), Marwa Peter Wangwe (wa pili kushoto), akihesabu dawa wakati akizikabidhi kwa Kamati ya Afya ya Kijiji cha Sanzawa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma juzi. Kutoka (kulia) ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uendeshaji wa zahanati hiyo, Iddi Degera, Mjumbe wa Kamati ya Afya ya kijiji hicho, Flaviana Joseph na Muuguzi Msaidizi wa Zahanati hiyo, Dativa Kiabuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo mpya taarifa za makandarasi waja

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kutengeneza mfumo wa 'Interpret Infrastructure System' (IIMS) ambayo itawawezesha kupata taarifa za kazi ambazo zinafanywa na makandarasi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mfumo huo utafungwa katika vifaa vya Wakala wa Barabara (Tanroads) ambavyo vinatumika katika ufanyaji kazi za miradi na kazi nyingine ambazo zitahitajika kufanywa katika za ujenzi.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, anayeshughulikia sekta ya ujenzi, Elius Mwakalinga, katika mkutano wa makandarasi jijini hapa.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka kubaini wizi unaofanywa katika kazi za miradi ambayo inaendelea katika maeneo mbalimbali.

Alieleza mfumo huo pia utafungwa katika vitendea kazi ambavyo vinatumiwa ikiwamo magari ili kubaini ubadhirifu unaofanywa katika kazi ambazo makandarasi wamekabidhiwa na serikali kuzifanya kwa manufaa ya jamii kwa ujumla.

"Sasa hivi tunatarajia kutengeneza mfumo huo lengo ni kutaka kuepusha rushwa katika taasisi mbalimbali pamoja na uchakuaji wa kazi zinazofanywa," alisema Mwakalinga.

Alibainisha hatua hiyo ni moja ya mkakati wa serikali baada ya kupata hasara ya raia wake kupoteza maisha katika vivuko, ikiwamo vivuko kuzama kutokana na kutokuwa na mfumo huo ambao unaonyesha kuwa mizigo imezidi, lakini wamiliki wanalazimisha hivyo hivyo ili wanufaike ilhali wanaiumiza jamii kwa ujumla.

Alisema mfumo huo utasaidia kujua uzito wa mizigo iliyopakiwa katika magari pamoja na kuona uzito uliozidi hata kama kwenye kivuko itajulikana na wao wataiona na kuwachukulia hatua atakayebainika anafanya hivyo. Aliongeza: "Unakuta mtu anakaa na ripoti ndani ya miezi mitatu ambayo anaweza kuibadilisha bila wahusika kujua, lakini kupitia mfumo huu utasaidia kujua nini kinafanyika na kuongeza kuwa ikiwekwa hiyo, kazi zitafanyika kwa ufasaha katika miradi waliopewa na serikali."

Awali, wakitoa malalamiko yao wakati wa mkutano huo, mkandarasi kutoka Mbeya, Kulwa Mayuma, alisema rushwa imekithiri sana katika sekta hiyo jambo ambalo linawafanya makandarasi washindwe kufanya kazi vizuri.

Alisema sekta hiyo imesahaulika kwa kiasi kikubwa na kuitaka serikali itupie jicho ili nao waweze kufanikisha kufanya kazi ambao wanakabidhiwa.

Naye Mwenyekiti wa Kampuni ya CATA ambaye ni mkandarasi, Oscar Munisi, alisema sekta imedharaulika kwa kiasi kikubwa sana na kusababisha makandarasi kuwekwa ndani bila sababu za msingi.

## Wakazi wa Nzuguni waondolewa hofu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewaondoa hofu wananchi wa Kata ya Nzuguni ya kubomolewa makazi yao kutokana na ujenzi usiozingatia taratibu za mipango miji baada ya kukamilisha zoezi la upimaji shirikishi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Godwin Kunambi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata hiyo iliyopo jijini hapa.

Alisema wamekamilisha zoezi la upimaji shirikishi eneo la Nzuguni 'A'.

"kwanza napenda kuwapongeza wataalamu wangu kwa kazi nzuri mliyoifanya ya upimaji shirikishi katika eneo za Nzuguni A, kupitia upimaji shirikishi, hofu kwa wananchi imeondolewa, kwamba kesho watabomolewa makazi yao," alisema.

Kunambi alisema kazi hiyo imetekelezwa na halmashauri kwa lengo la kuwahakikishia wananchi makazi bora na salama kwa mujibu wa taratibu za Mipango Miji.

Kunambi alisema kukamilika kwa zoezi la upimaji shirikishi kutawawezesha wananchi kupata hati halali za umiliki wa viwanja ambazo zitawawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha.

Alisema kuwa Halmashauri ya Jiji inadhamira ya kuona wananchi wake wanaishi katika makazi bora na kuwa na uwezo wa kifedha kupitia rasilimali zao ikiwamo ardhi.


Kuhusu migogoro ya mipaka kwa baadhi ya wananchi, aliwahakikishia wananchi hao kuwa timu ya wataalamu wa kutosha kutoka halmashauri wataweka kambi katika Kata ya Nzuguni ili kuhakikisha wananchi wote wenye changamoto wana hudumiwa na kugawiwa viwanja kwa mujibu wa taratibu.

Hata hivyo, aliwatakiwa wananchi hao kujiepusha na ununuzi wa mashamba bila kuzingatia taratibu za Mipango Miji na kupatiwa hati ya umiliki na muuzaji ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili kuepuka hasara.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma sasa ni makao makuu ya nchi, hivyo napenda kuwahakikishia kuwa sheria za ardhi zinasimamiwa barabara...Mtanzania yeyote asinunue shamba bila hati kwani ardhi au shamba au kiwanja hakikisha unapata hati ya umiliki," alisisitiza.

Naye msimamizi wa mradi wa upimaji shirikishi Nzuguni A, Aisha Masanja, alisema mradi huo utahudumia wananchi 5,942 ukiwa na jumla ya viwanja 11,160 vya matumizi mbalimbali.

Alisema mradi huo una faida kwa kuwa utawawezesha wananchi kujenga katika viwanja vilivyopimwa na kuwawezesha kupata hati za umiliki wa viwanja hivyo.





Mwananchi akiwa na mfuko wa taka akitupa mahali ambako sio sahihi na huku kukiwa na rundo la takataka lililotelekezwa kando ya barabara katika eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hospitali jeshi zapata mgawo dawa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amesema hospitali 13 zinazomilikiwa na vikosi vya ulinzi likiwamo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), zimeanza kupata mgawo wa dawa kutoka serikalini.

Hamad alisema wizara imechukua uamuzi huo baada ya kuridhishwa na huduma za vituo vya afya zikiwamo hospitali zinazomilikiwa na vikosi hivyo.

Alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema mgawo wa dawa zinazosambazwa katika vikosi vya ulinzi zitatolewa bure kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma za afya.

"Wizara ya Afya tayari tumeanza kutoa mgawo wa dawa kwa ajili ya hospitali za kijeshi ili kusaidia kutoa huduma kwa wananchi," alisema. Alizitaja hospitali zilizoanza kupata mgawo wa dawa kuwa ni Ali Khamis Camp ya JWTZ Pemba, KMKM iliyoko Bububu na Hospitali ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) iliyoko Saateni.

"Hospitali za vikosi vya ulinzi tumeanza kuzipatia mgawo wa dawa na zile za vikosi vya SMZ nazo zinafaidika na mgawo huo," alisema.

Mohamed alizipongeza kwa dhati hospitali za vikosi vya ulinzi kwa kufanya kazi kubwa kusaidia huduma za afya kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Alisema hospitali hizo zimekuwa na uhusiano mkubwa na wananchi, huku zikitoa huduma bora kwa wagonjwa wake.

# Ujenzi uwanja wa ndege, bandari kwa fedha za ndani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema miradi miwili mikubwa ya ujenzi wa jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na Bandari ya Mpiga Duri utatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani.

Waziri wa Ujenzi, Usafirishaji na Uchukuzi, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema hayo wakati akijibu hoja mbalimbali za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioachangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Dk. Sira alisema mradi wa ujenzi wa jengo la abiria (Terminal III) hadi sasa haujapata ufadhili baada ya Benki ya Exim kutoka China kushindwa kutoa fedha za kugharamia mradi huo.

Alisema baada ya kushindwa kupata fedha kutoka benki hiyo, serikali imeamua kutumia fedha zake za ndani kugharamia ujenzi huo.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume utatekelezwa kwa kutumia fedha zetu za ndani baada ya kukosa ufadhili," alisema.

Aidha, alisema ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri iliyoko eneo la Maruhubi, Unguja, utatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani zinazotokana na makusanyo ya kodi.

Waziri Sira alisema Bandari ya Mpiga Duri ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha huduma za mizigo na usafirishaji kutokana na Bandari ya Malindi kuzidiwa na utoaji wa huduma.

"Miradi hiyo miwili serikali imeamua kuitekeleza hatua kwa hatua kwa kutumia fedha zake za ndani, huku juhudi za kutafuta wafadhili zaidi kugharamia mradi huo zikifanyika," alisema.

Pia alisema serikali itaimarisha huduma za mawasiliano ya baharini kwa kununua boti tano zitakazotoa huduma kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo.

"Ahadi ya serikali kununua boti tano za kutoa huduma kwa abiria kwa wananchi wa Unguja na Pemba itatekelezwa kwa kwa kutumia fedha zetu," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, huku suala la ujenzi wa barabara za vijijini likipewa kipaumbele.

# Waziri apigia debe uchangiaji wa damu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, amewataka wananchi kuendelea kuchangia damu kwa hiari kwa kuwa mahitaji ya damu salama nchini yamekuwa makubwa.

Amesema mahitaji ya damu kwa mwezi ni wastani wa chupa 1,550 kwa matumizi ya kawaida na watumiaji wakubwa ni wajawazito, watoto, majeruhi wa ajali na wagonjwa wa upasuaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusiana na siku ya wachangiaji damu duniani ofisini kwake, Mnazi Mmoja, Waziri Hamad alisema kutokana na wananchi wengi kuhamasika kutumia hospitali na vituo vya afya, mahitaji ya damu yanaongezeka kwa kiasi.

Waziri huyo alizipongeza taasisi na vikundi vya hiari vinavyojitokeza kuchangia damu katika mabonanza yanayoandaliwa na kitengo cha damu salama na kwamba hatua hiyo imekuwa msaada mkubwa katika hospitali na vituo vya afya.

Aliahidi kuwa wizara itaendelea kushirikiana na taasisi za kijamii na vikundi mbalimbali vinavyojitolea kuchangia damu ili kuondoa tatizo hilo na kuokoa maisha ya wananchi.

Hamad alisema lengo kuu la siku ya wachangia damu ni kuwapongeza, kuwajali na kuwahamasisha wachangiaji na kuwashawishi wengine wapya ambao wanaweza kujitolea damu kwa hiari ili kuokoa maisha ya wengine.

Alisema Siku ya Wachangiaji Damu Duniani ndiyo siku aliyozaliwa mvumbuzi wa makundi ya damu, raia wa Australi, Dk. Karl Landsteiner, hivyo inapaswa kuenziwa.

Naye Meneja Uhusiano na Uhamasishaji wa Kitengo cha Damu Salama, Hamad Bakari Magarawa, alisema maadhimisho hayo ambayo hufanyika Juni 14 kila mwaka, kwa Zanzibar yatafanyika Mwanakwerekwe.

Hamad Bakari Magarawa alisema kaulimbiu ya Siku ya Wachangiaji Damu Duniani mwaka huu ni 'Damu kwa Wote'.

## Wafanyakazi TANICA wamuomba RC Gaguti

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAFANYAKAZI wa Kiwanda cha Tanganyika Instant Coffee Public Limited Campany (TANICA PLC) kilichopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wamemwomba mkuu wa mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, kusaidia upatikanaji wa ufumbuzi wa migogoro katika kiwanda hicho.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya Gaguti kufika kiwandani hapo kusikiliza changamoto za utendaji kazi na mienendo ya kibiashara na ustawishaji wa kampuni ya TANICA kwa msimu wa Mei 2018-Aprili 2019.

Wilison Kabwemela alisema, migogoro hiyo imekuwapo kuanzia mwaka 2000 hali iliyolazimu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuunda timu ya ufuatiliaji shughuli za kiwanda.

Alisema taarifa ya timu hiyo ilisababisha kuvunjwa uongozi uliokuwapo na kuwekwa mwingine, ambao matarajio yalikuwa ni kumaliza baina ya wafanyakazi na uongozi kutokana na kudai maslahi mbalimbali.

Aidha, alisema changamoto iliyopo kwa sasa ni kushuka kwa mtaji wa uendeshaji kiwanda baada ya kubainika kuwapo kwa matumizi mabaya ya ofisi na utendaji mbovu kwa baadhi ya wakuu wa idara na wafanyakazi.

"Kinacholeta makundi, hakuna na wafanyakazi hawana stahiki, na wengine tangu uongozi ulioko nje kuondolewa," alisema Kabwemela.

Enzi Mwambembe, alisema ukosekanaji wa uzalendo katika kazi umefamya wafanyakazi kutumia muda mwingi kutengeneza makundi yanayochafua kiwanda kwa kutengeneza mivutano.

Editha William alisema migororo hiyo huibuka kutokana na kutokuwapo mpangilio mzuri katika kazi, hali inayofanywa na viongozi unapotaka kutoa ajira zisizofuata usaili

Meneja Mkuu wa TANICA, Linus Leopold, alisema kampuni ilipitia wakati mgumu baada ya kulipia deni la Sh. milioni 671.7 lililopokelewa kutoka kwa watanguli wake.

Alisema kuwa kulingana na hali mbaya ya kifedha awali kumekuwa na kipindi kigumu ambacho kimesababisha kukosa mtaji wa kununulia malighafi kutoka mnadani.

Alieleza kuwa sasa malighafi zinapatikana kwa mkopo kutoka vyama vya ushirika Kagera Cooperative Union (KCU) 1990 Ltd na Karagwe District Cooperative Union (KDCU) Ltd vilivyomo katika mkoa.

"Malighafi tunazipata katika vyama vya ushirika hivyo, KDCU hutoa tani 90 iliyochakatwa kwa bei ya shilingi 3,200 kwa kilo moja, ikiwa kahawa ya maganda hununuliwa kwa shilingi 1,000 kwa kilo," alisema Leopold.

Hata hivyo alisema kwa msimu wa 2018/019, uzalishaji umekuwa kilo 251,130 ikiwa bajeti ilikuwa kilo 300,000 sawa na asilimi83.71kwa upande wa kahawa ya unga, kahawa ya kukaanga zimezalishwa kilo 484,133 bajeti ilikuwa kilo 600,000 sawa na asilimia 80.7

# Mapya ya Hashim Rungwe zuio la mikutano ya kisiasa

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Umma (Chauma), Hashim Rungwe, amedai zuio la mikutano ya siasa lililowekwa na serikali limewezesha vyama vya upinzani kuunganisha nguvu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Rungwe aliyegombea urais mara mbili, alisema kutokana na kuzuiwa na serikali kufanya mikutano ya siasa, sasa vyama vimelazimika kuungana ili kupambana kwa pamoja.

"Ukweli ni kwamba tumebanwa, na mimi pia nimebanwa kwa sababu nikiamua kwamba nataka niende kesho Kisarawe nikafanye mkutano siwezi kwenda hata kama nataka kwenda kufanya mkutano Ferry pale siwezi, sasa kutokana na kubanwa huko vyama vikaungana," Rungwe alisema.

Ikiwa imebaki miezi michache kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa Oktoba mwaka huu pamoja na uchaguzi mkuu mwakani, zuio la mikutano ya kisiasa bado limeendelea kuwa mwiba kwa vyama vya siasa hasa upande wa upinzani ambao umekuwa ukilalamika mara kadhaa.

Tangu kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa mwaka 2016 vyama vya siasa vimekuwa vikitoa matamko mbalimbali kupinga zuio hilo na kudai kuendelea na mikutano hiyo bila mafanikio ya utekelezaji wa maazimio hayo.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kilishatangaza kusudio la kufanya mikutano hiyo licha ya kupigwa marufuku na serikali tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wamwaka 2015, lakini ni miezi kadhaa sasa imepita bila utekelezaji wa azimio hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo (katikati), akionyesha hundi ya shilingi milioni tano, zilizotolewa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) Kituo cha Amani, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Muheza. Kulia ni Mkurugenzi wa Kituo hicho kilichopo wilayani humo, William Kisinza na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji wilaya hiyo, Davidi Kilua. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wataalamu kutoka India waja utekelezaji mradi mkubwa maji

**Na Steven William,** MUHEZA

WATAALAMU wa ushauri na usanifu kutoka India wameanza kazi ya usanifu wilayani Muheza mkoani Tanga kwa ajili ya maandalizi ya kuanza mradi mkubwa wa kupeleka majisafi na salama katika mji wa Muheza kutoka mto Pangani ambao utaanza utekelezaji wa ujenzi Septemba.

Wataalamu hao walifika juzi na kuongozana na mhandisi kutoka Wizara ya Maji, Nixoi Sanga na Meneja wa Mamlaka ya Majisafi Muheza Mjini, Elikana Kayungilo.

Wataalamu hao walikagua chanzo cha maji cha Mto Zigi, Tarafa ya Amani na chanzo cha maji cha Mto Pangani pamoja na maeneo mengine ya kujenga matangi ya maji kwa ajili ya ushauri na usanifu.

Akizungumza na Nipashe, Kayungilo alisema wataalamu hao wa ushauri na usanifu kutoka India wamefika kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Kayungilo alisema baada ya wataalamu hao kukagua vyanzo hivyo viwili vya maji watapeleka taarifa, na baadaye watakuja tena Muheza kutoa taarifa kwamba chanzo kipi kinafaa kupeleka maji kwa wananchi ambao wamekuwa na kero ya maji ya miaka mingi.

Kayungilo alisema kuwa mradi huo wa kupeleka maji katika mji wa Muheza utagharimu Dola za Marekani milioni 14.5 ambazo ni mkopo wa riba nafuu ambapo miji 19 nchini ipo katika mpango huo wa kupata maji kutoka katika fedha za mkopo wa India.

Wataalamu hao kutoka India Shiv Shamkar Prasad na Deepak Lakhampad kwa nyakati tofauti walisema kuwa wamefika kwa ajili ya kufanya kazi ya ushauri na usanifu katika mradi huo.

Mhandisi Sanga alisema kuwa wataalamu hao wamefika Muheza kufanya kazi hiyo na baada ya kumaliza, mkandarasi ataanza kazi ya kupeleka maji Muheza mjini kutoka katika chanzo cha maji mto Zigi ama mto Pangani.

Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, alisema kuwa kupatikana kwa mradi huo mkubwa wa maji utakuwa mkombozi wa kuondoa kero ya shida ya maji ambayo ilidumu zaidi ya miaka 50 sasa.

# Mradi taarifa za ardhi wazinduliwa

**Na Munir Shemweta, DODOMA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dorothy Mwanyika, amezindua mradi wa uanzishaji miundombinu ya upatikanaji taarifa za ardhi nchini.

Uzinduzi wa mradi huo ulifanyika jana katika ofisi za wizara, eneo la Mtumba jijini Dodoma na kuhusisha watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wawakilishi kutoka Benki ya Exim ya Korea.

Akizindua mradi huo, Mwanyika alisema uzinduzi wa kazi ya kusanifu uanzishaji miundombinu ya upatikanaji taarifa za ardhi nchini si tu utasaidia wananchi katika masuala ya umiliki wa ardhi bali utawezesha kubuni, kusanifu na kujenga miundombinu kama vile barabara, reli, majengo na miradi mikubwa.

Kwa mujibu wa Mwanyika, mradi huo utasaidia pia katika kukusanya mapato ya serikali kupitia sekta ya ardhi kwa kuwa maeneo ya wamiliki ya ardhi yatakuwa yameainishwa, hivyo kuwa rahisi wamiliki wake kutambulika na kusisitiza kuwa wizara yake itafanya kila jitihada kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa manufaa ya taifa.

Naye Mratibu wa Mradi huo, Erick Mwaikambo, alisema mradi huo utawezesha upatikanaji ramani za msingi na taarifa zinazowezesha upimaji ardhi kufanyika kwa haraka na kwa kasi na kwa bei nafuu na kuwezesha maeneo mengi nchini kupimwa pamoja na wananchi kupata miliki kwa urahisi.

Kwa mujibu wa Mwaikambo, mradi huo pia utasaidia upatikanaji ramani zitakazotumika kuandaa matumizi ya ardhi na hivyo kurahisisha kuwepo kwa miji iliyopangwa na kuondoa migogoro katika maeneo ya vijijini ikiwamo ile migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Mradi huo utasaidia pia shughuli za kubuni, kusanifu na kujenga miundombinu sambamba na kuwezesha kutunza mazingira na maliasili na sensa ya watu na makazi na hivyo kusaidia zoezi la kupiga kura wakati wa uchaguzi," alisema.

Mradi wa Kusanifu Uanzishaji Miundombinu ya Upatikanaji Taarifa za Ardhi nchini Tanzania unafadhiliwa na Serikali ya Korea kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi wa nchi hiyo na Benki ya Exim ya Korea (Korea Eximbank).

# Msako wa viwanda bubu kuzalisha plastiki waanza

**Na Beatrice Moses**

BAADA ya kufanikiwa katika utekelezaji wa katazo la utengenezaji, usambazaji na utumiaji wa mifuko ya plastiki, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), jana lilianza kampeni ya mtaa kwa mtaa jijini Dar es Salaam kubaini viwanda bubu vinavyotengeneza vifungashio visivyokidhi vigezo na viwango.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema NEMC imejipanga kuhakikisha wamiliki wa viwanda vyote bubu vinavyojihusisha na utengenezaji wa vifungashio visivyokidhi vigezo wanakamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara kutoka nje ya nchi wameonekana kukaidi katazo hili na kuendelea kuzalisha na kusambaza mifuko iliyopigwa marufuku jambo ambalo ni kinyume cha miongozo, kanuni na sheria ya mazingira," alisema Dk. Gwamaka.

Aidha, Dk. Gwamaka alifafanua kuwa kwa mujibu wa sheria mpya ya mazingira, watu ambao watazalisha au kuingiza nchini mifuko hiyo batili, faini yake ni kubwa na NEMC imejipanga kuisimamia sheria hiyo bila kupepesa macho.

"Sheria yetu ya mazingira imejieleza vizuri kuanzia kwa mzalishaji mpaka mtumiaji wa mwisho. Wazalishaji na waingizaji wa mifuko hiyo wanatozwa faini ya shilingi milioni kumi. NEMC tumejipanga kutekeleza sheria bila kujali rangi, dini wala nchi anayotoka mwenye kiwanda," alisisitiza.

Dk. Gwamaka aliongeza kuwa iwapo wazalishaji hao wanataka kuendelea kuzalisha vifungashio ni vyema wapate maelezo na vigezo ambavyo vinatumika katika kuzalisha mifuko hiyo kutoka Shirika la Viwango (TBS).

"Kwa kipindi hiki ambapo mwitikio wa mifuko mbadala umekuwa mkubwa, natoa rai kwa wenye viwanda bubu kufuata taratibu kwenda TBS ili kupata vibali na kuwa na uhalali wa kuendelea kuzalisha mifuko kulingana na vigezo ambavyo watapewa, tofauti na sasa ambapo mifuko hiyo haina 'label' yoyote."

Katika hatua nyingine, Dk. Gwamaka aliwashukuru Watanzania kwa kuitika mwito wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki kwa hiari na pasipo kulazimika kutumia nguvu ambazo zingewaathiri wananchi.

"Nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania kwa namna walivyounga mkono katazo hili bila ya serikali kutumia nguvu ya ziada na kwa wachache ambao wamekaidi tutashughulika nao kwa mujibu wa sheria," alisema.

NEMC wamejipanga kufanya ukaguzi wa viwanda vyote bubu ambavyo vimekaidi kutekeleza agizo la serikali kwa kuzalisha mifuko ya plastiki. Zoezi la ukaguzi linaanza leo jijini Dar es Salaam na kuendelea nchi nzima.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, akizungumza na wachimbaji madini ya green, kuhusu mikakati ya maendeleo, katika mkutano uliofanyika, eneo la Lemshuku Kata ya Komolo, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Magufuli aifagilia DRC kwa mchakato wa kidemokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, ameipongeza Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa kufanya mabadiliko ya uongozi kwa njia ya demokrasia.

Rais Magufuli alitoa pongezi hizo jana usiku wakati wa dhifa ya kitaifa iliyofanyika Ikulu kwa heshima ya Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, aliyewasili nchini kwa ziara rasmi ya kiserikali.

Aidha, alitumia fursa hiyo ya dhifa ya kitaifa Ikulu jijini Dar es Salaam, kumpongeza mgeni huyo, kwa kutimiza miaka 56 ya kuzaliwa jana.

Rais Magufuli alisema kuchaguliwa kidemokrasia ni historia kwa taifa hilo, kwa kuwa halikufanya uchaguzi tangu uhuru wake mwaka 1960.

Alimpongeza Rais Tshisekedi kwa hatua zake za kusaka amani ikiwamo kuyaunganisha makundi yote nchini humo, pamoja na kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa.

Alimhakikishia kiongozi huyo kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana na DRC, ikiwamo kuendelea kuiunga mkono kuhakikisha amani inapatikana.

Alisema Tanzania kupitia Umoja wa Mataifa, ilipeleka vikosi vyake vya kulinda amani, na kuwa vitaendelea kubakia huko ahadi amani ya kudumu itakapopatikana.

Alisema katika mchakato huo, askari 30 wa Tanzania wameshapoteza maisha.

Naye Rais Tshisekedi alimpongeza mtangulizi wake, Rais mstaafu, Joseph Kabila kwa jitihada zake za kupanua demokrasia zilizowezesha kubadilishana madaraka kwa njia ya kidemokrasia.

Alisema changamoto iliyobakia kwake ni kurejesha amani katika maeneo yote ya nchi hiyo. Viongozi hao watakutana leo na kufanya mazungumzo rasmi.

# Tozo 54 kufutwa TBS, TFDA

INATOKA UK. 3

Alisema hatua hiyo iliyolenga kuweka mazingira rafiki ya kibiashara na uwekezaji, inatarajiwa kupunguza mapato ya serikali kwa Sh. bilioni 2.5.

Kuhusu tozo za Shirika la Viwango (TBS), Dk. Mpango alisema anapendekeza kufuta tozo ya Sh. 50,000 ya maombi ya alama ya ubora, tozo ya nembo ya ubora ambayo ni asilimia 10 na 15 ya tozo ya gharama za mwanzo za ukaguzi wa ubora, tozo ya dhamana ya cheti cha kutumia nembo ya ubora na tozo ya asilimia 50 ya ununuzi wa fomu ya maombi ya bidhaa zinazotoka nje kwa bidhaa zote.

Tozo zingine zinazopendekezwa kufutwa katika shirika hilo ni za gharama za ujenzi ambazo hutozwa kulingana na umbali wa sehemu (mfano Dar s Salaam umbali wa Km tano ni Sh. 10,000) na tozo ya asilimia 0.2 ya gharama za mzigo na usafirishaji ya udhibiti wa vipodozi, vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kondomu, mabomba ya sindano, glavu, pamba na bendeji.

Alisema hatua hiyo inayolenga kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara, inatarajiwa kupunguza mapato ya serikali kwa Dola 20.

Akizungumzia tozo za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Mpango alisema anapendekeza kufuta tozo ya huduma za kusitisha kutoa kibali cha awali na kutoa kibali kipya inayotozwa kwa kiwango cha Dola 50 na tozo ya huduma ya kubadilisha taarifa za kibali inayotozwa kwa kiwango cha Dola 50.

Pia, anapendekeza kufuta tozo ya Dola 500 kwa ajili ya usajili wa kampuni ya Wakala wa Forodha kipindi cha usajili na kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa wasambazaji wakubwa Dola 1,000 na wasambazaji wa kati Dola 500 kwa mwaka.

Alisema serikali pia imependekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Majumbani na Viwandani Sura 182.

Waziri Mpango alisema marekebisho hayo yatahusisha kutoza tozo ya Sh. 40,000 ya usajili wa kemikali kwa kila kemikali kwa kipindi katika kipindi cha usajili badala ya Dola 20.

Pia kutoza kodi ya Sh. 200,000 kwa wafanyabiashara wakubwa na Sh. 50,000 kwa wajasiriamali wadogo kwa kila cheti cha usajili.

Alisema anapendekeza tozo ya Sh. 200,000 badala ya Dola 100 kwa wafanyabiashara wakubwa na Sh. 50,000 kwa wafanyabiashara wadogo kwa usajili wa eneo la kuhifadhia kemikali.

Dk. Mpango alisema hatua hiyo inatarajiwa kupunguza mapato ya serikali kwa Sh. milioni 450.

**SEKTA YA MIFUGO**

Waziri huyo alisema serikali imependekeza kufuta tozo mbalimbali kwenye sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na tozo ya Sh. 5,000 ya vibali vya vyombo vya kusafirisha maziwa chini ya lita 51.

Pia kufuta tozo ya Sh. 50,000 ya usajili wa vituo vya kukusanyia maziwa lita 201 kwa siku, tozo ya Sh. 5,000 ya usajili wa wazalishaji wa maziwa chini ya lita 51 kwa siku pamoja na kufuta tozo ya Sh. 500,000 ya usajili wa wasambazaji wa pembejeo za maziwa.

Alisema anapendekeza kufuta tozo ya Sh. 15,000 ya usajili wa wafugaji wadogo wa mifugo ya nyama na kufuta tozo ya Sh. 50,000 ya usajili wa wafugaji wadogo wa mifugo ya nyama.

Pia, kufuta tozo ya Sh. 50,000 ya usajili wa wafugaji wa kati wa mifugo ya nyama, kufuta tozo ya Sh. 75,000 ya usajili wafugaji wakubwa wa mifugo ya nyama na kufuta tozo ya Sh. 20,000 ya usajili wasimamizi wa minada ya awali.

Pia alipendekeza kufuta tozo ya Sh. 200 ya kibali cha kusafirisha kuku mkubwa nchini kubainisha kuwa hatua hiyo ya kurekebisha tozo katika sekta hiyo inatarajiwa kupunguza mapato ya serikali kwa Sh. bilioni 16.6.

# Mafanikio 17 ya awamu ya tano

INATOKA UK. 3

Alisema kazi zinazoendelea ni pamoja na majadiliano ya mkataba kati ya kampuni ya mradi na nchi hodhi.

**VIWANDA**

Waziri huyo alisema serikali katika kipindi hicho cha miaka mitatu na nusu iliendelea kusimamia utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alibainisha kuwa viwanda vipya 3,530 viijengwa katika mikoa mbalimbali ikijumuisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi (saruji, marumaru, nondo) na kilimo hususan kusindika matunda, mafuta na ngozi.

Alisema ujenzi wa viwanda vipya umechangia kupatikana kwa ajira mpya takriban 482,601 nchi nzima.

**KUHAMIA DODOMA**

Dk. Mpango (pichani) pia alisema serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka katika Jiji la Dar es Salaam kwenda katika Jiji la Dodoma.

Alisema Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na watumishi wa umma 8,883 kutoka wizara na taasisi wamehamia Dodoma na kwamba ujenzi wa ofisi za serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika na kuzinduliwa rasmi na wizara zote zimehamia na kuanza kutoa huduma.

**MADINI**

Kwenye sekta ya madini, Dk. Mpango alisema kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo la wafanyabiashara wa madini na kuendelea na ujenzi wa kituo cha pamoja eneo la Mirerani, serikali ikiamini uwekezaji huo utaimarisha upatikanaji wa takwimu na kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite.

Alisema mafanikio mengine katika sekta hiyo ni ujenzi wa jengo la taaluma la Chuo cha Madini (MRI) Dodoma, uanzishwaji wa masoko mikoani katika kuhakikisha wachimbaji wa madini wanapata masoko rasmi na serikali kupata mapato stahiki na ufungwaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu.

**ELIMU**

Kuhusu sekta ya elimu, Waziri Mpango alisema serikali imeendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa elimu msingi bila ada kwa kutoa Sh. bilioni 24.4 kila mwezi.

Alisema juhudi hizo zimechangia ongezeko la wanafunzi waliondikishwa darasa la kwanza kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,670,919 mwaka huu na kidato cha kwanza kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 710,436 mwaka huu.

Alisema mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta hiyo ni ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa shule za msingi 219 na sekondari 285 katika mikoa yote pamoja na ujenzi wa miundombinu ya vyuo vya ualimu saba.

**NISHATI**

Waziri Mpango alisema taifa limeshuhudia kuongezeka uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka MW 7,092.13 mwaka 2015/16 hadi MW 7,374 mwaka 2018/19.

Alisema hali hiyo imewezesha kuongezeka upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuongezeka kasi ya kusambaza umeme, akibainisha kuwa hadi kufikia Mei mwaka huu, jumla ya vijiji 7,127, taasisi za elimu 3,165, maeneo ya biashara 3,451 na pampu za maji 210 zimeunganishwa umeme.

**KILIMO**

Kuhusu sekta ya kilimo, Waziri Mpango alisema kiwango cha ukuaji wake kiliongezeka kufikia asilimia 5.3 mwaka jana ikilinganishwa na asilimia 4.8 kwa mwaka juzi.

Alisema ukuaji huo umewezesha kuongezeka kwa usalama wa chakula, kupungua kwa mfumuko wa bei ya chakula kufikia asilimia 2.7 Aprili mwaka huu kulinganishwa na asilimia 7.3 ya Aprili mwaka 2016.



**HUDUMA ZA AFYA**

Dk. Mpango alisema huduma za afya zimeimarika nchini kutokana na kununuliwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kupitia Bohari ya Dawa na kusambazwa katika vituo vya umma. Alisema upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94.4.

**HUDUMA ZA MAJI**

Waziri huyo alisema miradi 1,659 ya maji imekamilika kuwezesha kuongeza vituo vya kuchotea maji kufikia 131,370 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi milioni 25.3.

Alisema upatikanaji wa huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam umefikia asilimia 85, katika mikoa mingine umefikia asilimia 80, miji midogo asilimia 64 na vijijini asilimia 64.8.

**VIWANJA VYA NDEGE**

Dk. Mpango alisema mafanikio yaliyofikiwa katika eneo hilo ni kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na miundombinu yake yenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka, ukarabati wa Uwanja wa Ndege Dodoma, Tabora (awamu I na II) na Bukoba.

Alisema kazi zinazoendelea ni ufungaji wa rada nne za kuongoza ndege za kiraia JNIA, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) Mwanza na Songwe, akibainisha kuwa JNIA umefikia asilimia 95, KIA asilimia 90 na Mwanza asilimia 50.

**BANDARI**

Dk. Mpango alisema mafanikio yaliyofikiwa katika bandari ni ujenzi wa gati Na. 2 katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza kima chake.

"Vilevile, upanuzi wa Bandari ya Tanga na Mtwara umefikia asilimia 86 na 50 kwa mtiririko huo," alisema.

**BARABARA, MADARAJA**

Dk. Mpango alisema serikali ya awamu ya tano imefanya uwekezaji mkubwa katika kujenga na kukarabati barabara nchini ili kuhakikisha maeneo yote yanafikika kwa uhakika mwaka mzima.

Alisema juhudi hizo zitasaidia kuchochea kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji wa pembejeo na malighafi kwenda maeneo ya uzalishaji pamoja na usafirishaji wa mazao na bidhaa zingine katika maeneo mbalimbali ya masoko nchini.

**MELI MAZIWA MAKUU**

Dk. Mpango alisema kwenye Ziwa Victoria kunaendelea ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo, ujenzi wa chelezo na ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama.

Waziri huyo pia alisema makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti zilizoko katika Ziwa Victoria wamepatikana na uandaaji wa mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli tajwa umekamilika.

Aliongeza kuwa kwenye Ziwa Tanganyika, mikataba ya ujenzi wa meli mpya moja yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 400 na ukarabati wa meli ya MV Liemba umekamilika.

# Serikali yarejesha kodi taulo za kike

INATOKA UK. 2

kwenye gharama za kukausha nafaka kwa ajili ya kuzihifadhi. Aidha, hatua hii itachochea ukuaji wa kilimo cha mazao ya nafaka," alisema.

Aliongeza kuwa anapendekeza kupunguza kiwango cha VAT kutoka asilimia 18 hadi sifuri kwenye huduma ya umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar ili kuwapunguzia gharama za maisha wananchi wa Tanzania Zanzibar.

"Serikali iliridhia na kuelekeza kuwa umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania visiwani utozwe VAT kwa kiwango cha asilimia sifuri," alisema.

Waziri huyo pia alisema anapendekeza kutoa msamaha wa VAT kwa vilainishi vya ndege vinavyoingizwa nchini na waendeshaji wa ndani, Shirika la Ndege la Taifa au mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma ya Anga.

"Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini mikataba ya kimataifa ya huduma za anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwapo kwa msamaha huo," alisema. Waziri huyo pia alisema anapendekeza kusamehe VAT kwenye tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenye nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya shirika la ndege husika. "Tunapendekeza kufanya marekebisho ya sehemu ya pili ya Jedwali la VAT ili kuongeza kipengele kipya kinachotoa msamaha pale vinapoingizwa nchini na mashirika ya ndege yanayotambuliwa katika mikataba ya kimataifa ya huduma za anga," alisema.

Alisema hatua hiyo itawezesha nchi kutia saini mikataba ya kimataifa ya huduma za anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwapo kwa msamaha huo. Mpango alisema hatua hiyo ya marekebisho katika VAT inatarajiwa kupunguza mapato ya serikali kwa kiasi cha Sh. bilioni 1.647.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.


**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz ,au piga simu: 0767 223311

## CHETI KIMEPOTEA



**MAKAYA LUGISA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0333-114** kilichotolewa na MWANZA SEKONDARI mwaka 1990. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/59088/2019.**

115273702


## CHETI KIMEPOTEA



**ELIZABETH PHINEAS MAJIGWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0989-0009** kilichotolewa na KIBARA SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **BND/RB/2591/2019.**

215273802

## KUPOTEA KWA CHETI



**Khamis Juma** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0620-0083** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1998, katika shule ya Sekondari Tegata. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/STA/RB/57113/2019**

115272802


## KUPOTEA KWA CHETI



**Repha Japhet Malamba** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0316/0087** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1993, katika shule ya Sekondari KIbasila. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/STA/RB/59090/2019**

115272902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Said Kirumo** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0311-252** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1992, katika shule ya Sekondari Forodhani. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **STK/RB/9117/2015**

115272502

## GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR
LOW DENSITY AREA
BLOC "C",
PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
***(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)***

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 44/2019**

**Ombi la WITMAN JOSEPH NYASURU kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu LASTON A. KUMWENDA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/7/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 12/6/2019

215273302

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ERNEST ALBERT MWITA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T 989 DJX** Chassis No. **JTI725C1100209775** Yenye rangi ya Silver. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya Polisi: **MZR/TR/A.22/9/VOL.63/06**

215273202

## Taarifa ya Kufungwa/ Kufutwa kwa Kampuni

**INATOLEWA TAARIFA KUWA** katika mkutano wa ziada wa **JW SEAGON & CO INSURANCE BROKERS (TANZANIA) LTD** uliofanyika siku ya 30th November 2017, azimio maalum lilipitishwa kwa pamoja na wamiliki/wanahisa wa kampuni la kufunga kampuni kwani haikuweza endelea kufanya shughuli zake.

Ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni, wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

**Karimjee Attorneys
P.O. Box 76421
Dar es Salaam**

115274602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DELILAH MGAYA RASMUSSEN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T 892 ARQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAW/TR/RB/244/2019.**

115273902

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.**

**Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA**

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 16/06/2019 kampuni ya **Mselle Civil Engineers Co. Ltd** itasafirisha mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka MLANDIZI kuelekea MBWEWE kwa kutumia gari yenye namba za usajili: **T.670 DPD** gari linalosafirisha namba za usajili **S.TH2712, STH2782**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - **Urefu - M 9.7**
   - **Upana - M 2.5**
   - **Kimo - M 3.3**
3. Njia itakayopitia: **MLANDIZI** hadi **MBWEWE** kupitia **CHALINZE.** Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115272102

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.**

**Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA**

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 14-06-2019 kampuni ya BUSINESS **TRUST TANZANIA LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea ARUSHA kupitia BAGAMOYO, gari hilo lenye namba za usajili: **T 908 DGB / T 854 CLY**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - Urefu 19.00
   - Upana 2.88
   - Kimo 5.10
3. Gari hizo zinatoka **DAR ES SALAAM kuelekea ARUSHA** kupitia **BAGAMOYO.** Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115274202

## KUPOTEA KWA KADI

**Mlopa I. Sadallar** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba **MC 257 BYG** aina ya **BOXER,** Yenye chasis namba **MD2A2IBYXJWM85604.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KMR/RB/9140/2019**

115273502

## KUPOTEA KWA KADI

**Tanzania China Trade & Tourism Development** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba **MC 956 AHW** aina ya FEKON, Yenye chasis namba **LDAPAJOB7EGB24274.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KMR/RB/16654/2018**

115273602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GILAYO ELIDADI MAYUGI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAUM yenye namba za usajili **T 104 DND.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAW/RB/245/2019.**

115274002

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# REAL MADRID YAMSAJILI MENDY

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imekamilisha usajili wa beki wa kushoto kutoka Lyon, Ferland Mendy kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 48, huku kukiwa na kipengele cha kuongezwa euro milioni 5, mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, wametangaza.

Ujio wa mchezaji huyo mpya, unaibua mashaka kwa nahodha msaidizi wa Madrid, Marcelo mwenye umri wa miaka 31, huku kinda Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 22, anaweza kutolewa kwa mkopo kwa msimu wa 2019-20.

Theo Hernandez mwenye umri wa miaka 21, hatarajii kuwa kwenye mipango ya kocha, Zinedine Zidane msimu huu.

Mendy alifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho tatu katika mechi 44 alizoichezea Lyon msimu uliopita, hali iliyowaibua Manchester City na Barcelona kuwania saini yake pia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ametengeneza nafasi 40 katika mechi 30 za Ligue 1 pale Lyon msimu uliopita, wakati mabeki wa kushoto wa Real Madrid kwa pamoja wametengeneza nafasi 50 katika mechi 38.

Madrid tayari imemsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Serbia, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 21, kutoka Klabu ya Eintracht Frankfurt kwa euro milioni 60, beki wa Brazil, Eder Militao mwenye umri wa miaka 21 kutoka Porto kwa euro milioni 50 na mshambuliaji wa Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 18 kutoka Santos kwa euro milioni 54.

Mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 28, pia alisajili hapo Madrid wiki iliyopita wakati Zidane akiwa kwenye harakati za kukifumua kikosi hicho.





# GUARDIOLA: SITAPUMZIKA KUFUNDISHA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amekanusha madai kwamba ana mpango wa kuchukua likizo ya muda kufundisha soka.

Baada ya kushinda mataji mawili ya Ligi Kuu England, pamoja na FA na Ngao ya Jamii katika miaka yake mitatu pale Manchester City, ripoti zilidai kwamba, Guardiola anaweza kupumzika kama akishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 48 alichukua maamuzi kama hayo ya kupumzika kufundisha wakati alipoondoka Barcelona kabla ya kuchukua mikoba pale Bayern Munich mwaka 2013.

Akizungumza na gazeti la Marca la nchini Hispania, Guardiola alisema: "Hapana. Sitachukua mapumziko. Mimi ni kijana na bado nataka kuendelea kufundisha soka."

"Habari zinazoandikwa na vitu vingine vingi sio vya kweli. Kama hawatanifukuza, nitaendelea kubakia pale." City imeshindwa kusonga mbele zaidi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu Guardiola kuchukua mikoba ya kuinoa.

# PSG wakaribia kumnasa De Ligt



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imebainisha kwamba, inakaribia kumsajili Matthijs de Ligt kutoka Ajax, huku wakala wa beki huyo, Mino Raiola kwa sasa akiripotiwa kuwa yupo jijini Ufaransa, ESPN FC imebainisha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amekuwa ndiye anayetajwa zaidi kwa usajili kipindi cha majira ya joto kwa klabu kadhaa kubwa Ulaya kuonekana kuisaka saini yake.

Klabu kama Barcelona na Juventus zimekuwa zikiisaka saini yake kwa udi na uvumba, lakini mabingwa hao wa Ligue 1 wanaonekana kukaribia kukamilisha usajili wa mchezaji huyo kwa ada inayotajwa kuwa ni euro milioni 75.

ESPN FC imebainisha kwamba, Barca walikuwa wametoa ofa yao ya mwisho mwanzoni mwa wiki hii, lakini hilo halijamzuia Raiola kufanya mazungumzo na PSG.

Raiola aliwasili jijini Paris Jumatano kwa ajili ya kujadiliana maslahi binafsi ya De Ligt na PSG na huku mshahara wake ukitajwa kuwa ni euro milioni 12 kwa mwaka.

Na pia inadaiwa De Ligt mwenye umri wa miaka 19 atasaini mkataba wa miaka mitano na mabingwa hao wa Ufaransa.

Kama De Ligt akikubali kujiunga na PSG atakuwa mmoja wa wachezaji ambao wanalipwa fedha nyingi zaidi, baada ya Neymar ambaye kwa msimu uliopita peke yake alitia mfukoni euro milioni 66.

HABARI MICHEZO



# GRIEZMANN

## ATASAINI BARCA, ASEMA BOSI WA ATLETICO

**MADRID, Hispania**

OFISA Mtendaji wa Atletico Madrid, Miguel Angel Gil Marin, amesema kwamba Antoine Griezmann ataichezea Barcelona msimu ujao, kwa mujibu wa ESPN FC.

Griezmann mwenye umri wa miaka 28, aliwasiliana na Atletico kuwa anaondoka kipindi hiki cha majira ya joto klabuni hapo ikiwa ni wiki ya mwisho kuelekea mwishoni mwa msimu huu wa Hispania, La Liga.

Wakati huo, vyanzo pale Barcelona viliiambia ESPN FC kwamba mabingwa hao wa Hispania walikuwa na matumaini makubwa ya kumsajili mshambuliaji huyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa bado hajabainisha wapi atakuwapo msimu ujao, licha ya kutamka hadharani kuondoka kwake Atletico, lakini Gil Marin hana shaka naye wapi anapokwenda.

"Ninajua wapi Griezmann atacheza msimu ujao tangu Machi," amesema Gil Marin akiiambia televisheni ya Movistar juzi Jumatano. "Ataichezea Barcelona."

Griezmann ameibua mjadala hivi karibuni kuhusu wapi atakapocheza, huku klabu ya Paris Saint-Germain ikitajwa kwamba nayo ipo kwenye mbio za kuwania saini yake.

Na akanukuliwa akisema kuwa, yeye anajua wapi atacheza msimu ujao na kusema watu wawe na subira.

"Nataka majaliwa yangu kuamua mwenyewe na si mtu mwingine, lakini kuweni na subira," alisema Griezmann Jumanne wiki hii.

"Pengine ndani ya wiki mbili tutajua kitu fulani, kwamba wapi nakwenda na ninacheza msimu ujao."

# ALGERIA YAMTIMUA NYOTA WAKE

**CAIRO, Misri**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Algeria, Haris Belkabla, ameondolewa katika kikosi hicho baada ya kuonekana mtandaoni katika kipande cha video akishusha suruali na kuonyesha sehemu ya makalio mbele ya wachezaji wenzake.

Belkebla ambaye anachezea klabu ya Stade Brestois ya Ufaransa alikuwa ameitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi hicho kinachoshiriki michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019).

Video hiyo iliyosambaa imeripotiwa kuwa ilichukuliwa wakati wakiwa hotelini.

Nafasi ya Belkebla imechukuliwa na Mohamed Benkhemassa anayechezea klabu ya USM Alger.

Algeria imepangwa katika Kundi C katika michuano hiyo itakayoanza mwezi huu nchini Misri na itachuana na Tanzania, Senegal na Kenya.

"Kocha Djamel Belmadi aliamua kumwondoa Belkebla kwenye kikosi cha Taifa kutokana na tukio hilo la utovu mkubwa wa nidhamu. Kocha amechukua uamuzi huo ili kuhakikisha wachezaji wanakuwa na nidhamu," Shirikisho la Mpira wa Miguu la Algeria limeeleza kwenye taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ameomba radhi kwa wachezaji na taifa lake kwa ujumla kutokana na tukio hilo ambalo ameliita la aibu.

"Ninaomba radhi kwa watu wa Algeria. Sikuwa nafahamu niko 'live' kwenye mitandao ya kijamii. Hata hivyo, kitendo nilichokifanya hakikuwa sahihi," amesema.

"Nimefanya kosa na nimelipa gharama. Imenivunja moyo wangu. Ninatumaini Algeria itashinda AFCON, lakini ndoto yangu imeishia hapa," ameongeza.

Ingawa ilikuwa mara ya kwanza kuchezea timu hiyo, kiungo huyo amewahi kushiriki kwenye kikosi cha taifa cha vijana wenye umri chini ya miaka 23.




# United yakamilisha usajili wa James

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imekamilisha usajili wa mchezaji wa kimataifa wa Wales, Daniel James kutoka Swansea kwa mkataba wa miaka mitano, huku kukiwa na kipengele cha kumwongezea miezi 12 mingine.

Klabu hiyo ya Old Trafford imetangaza kuwa wamefikia makubaliano ya kumsajili James, kwa ada ya awali ya pauni milioni 15, huku kukiwa na uwezekano wa kuongezeka hadi pauni milioni 22.

Uhamisho hivi sasa umekamilika kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ukiwa ni usajili wa kwanza kwa United kipindi hiki cha majira ya joto.

Na pia ni usajili wa kwanza tangu Ole Gunnar Solskjaer achukue mikoba ya kocha, Jose Mourinho Desemba mwaka jana.

"Daniel ni winga kijana anayevutia, kwani ana kipaji, akili pamoja na kasi akiwa dimbani," amesema Solskjaer.

"Alikuwa na msimu bora akiwa na Swansea City na ana kila kitu kinachomfanya kuwa mchezaji wa Manchester United.

"Tunafuraha kukubali kusaini na klabu yetu na tunasubiria kwa hamu kuona kipaji chake uwanjani akiisaidia timu yetu. Hapa kuna mazingira mazuri ya kumfanya Daniel kuendelea kuimarika."

Kwa upande wake James amesema: "Hii ni moja ya siku zangu bora katika maisha yangu na yenye changamoto kubwa, naangalia uwezekano wa nini kitaendelea.

"Ligi Kuu England ni ligi bora duniani na Manchester United ni sehemu sahihi kwangu kuwapo hapa na kuendelea kuimarika kama mchezaji."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HUDSON-ODOI AIPA MASHARTI CHELSEA

Ni endapo atakubali kumwaga wino wa kuendelea kuitumikia...

**LONDON, England**

MCHEZAJI kinda wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, ametoa masharti kwa klabu yake hiyo kuwa kabla ya kutia saini mkataba mpya kipindi hiki cha majira ya joto.

'Dogo' huyo amesema hatamwaga wino hadi ahakikishiwe namba katika kikosi cha kwanza vinginevyo ataondoka klabuni hapo.

Hudson-Odoi anawindwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya baada ya kucheza kwa kiwango bora msimu uliopita.

Mazungumzo ya Chelsea na winga huyo kinda mwenye miaka 18 kuhusu mkataba mpya yanaendelea.

"Jambo la msingi kuliko yote ni kupata nafasi ya kucheza, hicho ni kitu ambacho kila mchezaji huwa anakifikiria kwenye akili yake na mimi ndio nataka iwe hivyo nihakikishiwe kabla ya kusaini mkataba mpya," amesema Hudson-Odoi akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

Hudson-Odoi ameongeza kusema kwamba, bado ana mapenzi na Ligi Kuu England, lakini la msingi zaidi kwake ni kupata nafasi ya kucheza, kwa sababu maisha yake ni kucheza soka, hakuna jingine analowaza.

"Mimi ni mchezaji, haina maana kama sitapata nafasi ya kucheza, kwa sababu ili niitwe mchezaji ni lazima nipate nafasi ya kucheza mara kwa mara, na sio kukaa benchi," alisema.

Hudson-Odoi amesita kuongeza mkataba kwa kuhofia kusugua benchi msimu ujao kama ambavyo ilimtokea msimu uliomalizika, kwani alipata nafasi chache za kucheza.

Hudson-Odoi alionyesha mchezo mzuri baada ya kocha Maurizio Sarri kumpa nafasi katika kikosi cha kwanza ambapo alifunga mabao matano kabla ya kuumia katika mechi dhidi ya Burnley.

"Mimi sina tamaa ya fedha, jambo muhimu kwangu ni kupata namba kikosi cha kwanza, vinginevyo sitakubali kutia saini," alisema.

Mchezaji huyo amekuwa akiwaniwa na miamba ya soka la Ujerumani, Bayern Munich kwa muda mrefu na imeshatuma ofa yake kwa ajili ya kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto, ambapo ilikataliwa na Chelsea.

Hata hivyo, ni wazi kwamba uwezekano wa Hudson-Odoi kukubali kusaini mkataba mwingine ni mdogo, kwani kilio chake yeye ni namba kwenye kikosi cha kwanza.

## KWA UFUPI

### GRIEZMANN KUTUA BARCA

BOSI mkuu wa Atletico Madrid, Miguel Angel Gil Marin, amethibtisha kuwa straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann (28), atajiunga na Barcelona katika kipindi cha majira ya moto. ***(Sport)***

### GRIEZMANN AGOMBEWA

MANCHESTER United inataka iwasilishe ofa ya kumwania mshambuliaji, Antoine Griezmann na imesema iko tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 95 ili kumnasa Mfaransa huyo. ***(Sun)***

### GUARDIOLA: SIPUMZIKI

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekanusha taarifa zinazosambaa kuwa anajiandaa kupumzika kufundisha soka mwishoni mwa msimu ujao. ***(Independent)***

### FEKIR ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imerejea katika mbio za kuwania saini ya kiungo mchezeshaji wa Lyon, Nabil Fekir, lakini hawatalipa dau la pauni milioni 53 ambalo linatakiwa na klabu hiyo ya Ligue 1 ili kumuuza Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Le Progres, via Mail)***

### JUVE WAMFATA SARRI

MKURUGENZI wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici, amewasili jijini London ili kukamilisha mchakato wa kumnasa Kocha wa Chelsea Mtaliano Maurizio Sarri. ***(Calciomercato)***

### CHELSEA YAKOMAA

CHELSEA imeweka wazi kuwa haitatoa kibali cha kumruhusu Maurizio Sarri kuondoka Chelsea mpaka pale mabingwa wa Italia, Juventus watakapokubali kulipa kaisi cha fedha watakachokubaliana ili kuvunja mkataba. ***(Mail)***

### PALMIERI AIKATAA JUVE

BEKI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Italia, Emerson Palmieri ambaye ana umri wa miaka 24 anahusishwa na tetesi za kujiunga na Juventus amesema anafuraha kuona anabakia klabuni hapo Stamford Bridge. ***(Star)***

### LIGT WA PSG

WAKALA wa Matthijs de Ligt, Mino Raiola amekutana na Mkurugenzi wa Michezo wa Paris St-Germain, Antero Henrique kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo ya usajili wa beki huyo wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi. Klabu hizo mbili zinakaribia kufikia makubaliano ya ada ya pauni milioni 66.6. ***(RMC Sport - in French)***

### LIGT ATENGEWA KITITA

MABINGWA wa Ufaransa, Paris St- Germain wamempa ofa ya thamani ya pauni milioni 10.6 beki wa Ajax, Matthijs De Ligt ambayo itakuwa ni ya miaka mitano. ***(ESPN)***

### FORNALS MAMBO SAFI

WEST Ham iko katika hatua za mwisho za kunasa saini ya kiungo mshambuliaji wa Villarreal Mhispania, Pablo Fornals ambaye thamani yake ni pauni milioni 24 ifikapo mwishoni mwa wiki hii. ***(Guardian)***

### NDOMBELE KITAELEWEKA

KLABU ya Tottenham inakaribia kukamilisha usajili wa kiungo wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tanguy Ndombele (22), kwa dau la pauni milioni 66.6. ***(Guardian)***

### LOVREN ANUKIA MILAN

AC Milan imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Croatia, Dejan Lovren ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***



## HABARI MICHEZO

# NDAYIRAGIJE AJIPANGA KUIPAISHA AZAM BARA



Etienne Ndayiragije,

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA mpya wa mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC Mrundi Etienne Ndayiragije, amesema amejipanga kuifanya timu hiyo kuwa bora katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Azam FC iliyomaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita katika nafasi ya tatu, pia ni mabingwa wa mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ndayiragije, alisema kuwa anaamini mapendekezo yake yakitelekezwa vema, Azam FC itakuwa ni timu bora na inayotoa ushindani katika mashindano yote watakayoshiriki.

Ndayiragije alisema kuwa anataka kuona Azam FC inapata heshima kwa kufanya vema na kushangiliwa na idadi kubwa ya mashabiki kama zilivyo timu nyingine.

"Hata hizo klabu zenye mashabiki wetu sasa hivi zilianza kama Azam, naamini na yenyewe itafika huko, ni mipango na programu zikifanyika vema, hakuna kinachoshindikana katika ulimwengu huu," alisema kocha huyo. Alieleza kwamba anahitaji ushirikiano na kuona wachezaji wanajituma wakati wote wanapokuwa kwenye mashindano ili waweze kufikia malengo ya pamoja.

Ndayiragije, kocha wa zamani wa Mbao FC ya jijini Mwanza na KMC ya jijini, amerithi mikoba iliyoachwa na Mholanzi, Hans van der Pluijm ambaye alitemwa na mabosi wa timu hiyo baada ya kupata matokeo mabaya.

Mtihani wa kwanza wa Mrundi huyo itakuwa ni kutetea taji la Kombe la Kagame ambalo wanalishikilia kwa mwaka wa pili mfululizo.

Kikosi cha Azam FC kinatarajia kuanza mazoezi kujiandaa na michuano hiyo ifikapo Julai 18 mwaka huu, na tayari ilishawapa mikataba wachezaji wake inaowahitaji katika msimu ujao.




Nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, Ofisa wa Benki ya DTB, Dennis Rauya (nyuma kulia), wakiwa pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Kijitonyama jijini Dar es Salaam baada ya kumaliza mafunzo ya mchezo wa soka yaliyofanyika hivi karibuni. DTB kwa kushirikiana na Samatta iliandaa mafunzo yao ili kuwapa mbinu za msingi wachezaji hao chipukizi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mshana: Dua zote kwa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Asumpter Mshana, amewataka Watanzania kuwa wazalendo, kuonyesha mapenzi na kuiombea dua Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambao inajiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) ili iweze kufanya vema.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mshana alisema katika kipindi hiki Watanzania wanapaswa kuungana kuiombea timu yao ili ifanye vizuri kwenye mashindano hayo na kuipa heshima jina la nchi.

**"Sisi tunachotaka ni kikombe, wachezaji wawe wale wale au wengine sisi hatuangalii mtu, tunachoangalia ni kurudi na ushindi," alisema Mshana.**

Kiongozi huyo aliwaasa wachezaji walioachwa kwenye kikosi hicho na wao wanatakiwa kuiombea Stars irejee na ushindi, badala ya kunung'unika.

"Siku zote kuna next time (wakati mwingine), kama kuna mtu umebaki, unatakiwa kuanza kuiombea timu yetu ya Tanzania ili turudi na ushindi," alisisitiza Mshana.

Fainali za Afcon zinatarajiwa kufanyika kuanzia Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu, ambapo mataifa 24 yatapambana kuwania ubingwa huo.

Tayari Kocha Mkuu wa Stars, Emmanuel Amunike, ameshawasilisha majina ya wachezaji 23 ambao watapeperusha bendera ya Tanzania katika fainali hizo ambazo timu hiyo ilikosa kushiriki kwa miaka 39.

Stars iko katika Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na majirani zao Harambee Stars ya Kenya.

# Shotokan Karate kuchaguana Julai 27

**Na Getrude Mpezya**

CHAMA cha Mchezo wa Shotokan Karate Tanzania (TASHOKA) kinatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu ifikapo Julai 27 mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Akizungumza jana jijini, Ofisa Habari wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Frank Mgunga, alisema kuwa tayari fomu kwa ajili ya wadau wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali zimeanza kutolewa katika ofisi za baraza hilo.

**Mgunga alisema kuwa baada ya kukamilika kwa mchakato wa kurudisha fomu, wagombea wote watakaokuwa wamejitokeza wanafanyiwa usajili na watakaopita, watapitishwa kuwania nafasi ambazo wameomba.**

Alizitaja nafasi ambazo zitawaniwa katika uchaguzi huo ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

"Ili kupata fomu, mgombea anatakiwa kufanya malipo ya Sh. 50,000 katika akaunti ya baraza kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya serikalini kwa kutumia namba ya utambulisho wa malipo husika," alisema Mgunga.

Alieleza mojawapo ya sifa ya mtu anayetaka kugombea katika uchaguzi huo ni kuwa na uzoefu kwenye mchezo huo na vile vile kukubali kujitolea kufanya shughuli mbalimbali za chama hicho.

"Tunawaomba wadau waje kuchukua fomu kuwania nafasi za uongozi, ili tupate viongozi watakaosaidia kushiriki katika maendeleo ya mchezo huu hapa nchini," Mgunga aliongeza.

Michezo
Ijumaa Juni 14, 2019
Nipashe



## Hudson-Odoi aipa masharti Chelsea

HABARI UK 30



Nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta (kulia), akiwa na wachezaji wenzake wa timu hiyo wakifanya mazoezi kujiandaa na fainali za Kombe la Afrika (Afcon 2019), zitakazofanyia Misri baadaye mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAIZIDI UJANJA YANGA

●●● Yafanikiwa kumbakisha Mkude klabuni hapo, yatamba kusajili 'majembe' ya viwango...

**Na Somoe Ng'itu**

KWA mara nyingine, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameendelea kuwazidi maarifa watani zao Yanga baada ya kufanikiwa kumpa mkataba mpya kiungo wake, Jonas Mkude, imefahamika.

Mkude ambaye wiki iliyopita alitemwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuendelea kuwatumikia mabingwa hao na kuzima ndoto za Yanga ambao walikuwa wanawania saini ya kiungo huyo.

Nyota wengine wa Simba ambao tayari wameshasaini mikataba mipya ni pamoja na golikipa, Aishi Manula, Erasto Nyoni na nahodha, John Bocco, ambaye bado mkataba wake umegubikwa na utata baada ya klabu nyingine ya Afrika Kusini, Polokwane City ikisema kwamba inamtambua ni mchezaji wake halali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema jana kuwa klabu hiyo itaendelea kuweka wazi taarifa za wachezaji wa ndani iliyowasajili kila siku, na kuanzia wiki ijayo wanawatangaza nyota wa kigeni ambao wamekamilisha mazungumzo ya kuwasajili.

> **"Kila siku ikifika saa 7: 00 mchana, tutakuwa tunadondosha mmoja mmoja, ila kuanzia wiki ijayo tutaanza kwa mfumo mwingine , tutawatambulisha majembe yetu ya nje," alisema Magori.**

Aliongeza kuwa mwaka huu Simba itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.3 ambao walitumia katika msimu uliopita kwa sababu wanahitaji kupata mafanikio.

Alisema pia imeanza maandalizi kwa ajili ya 'Wiki ya Simba' itakayohitimishwa na Tamasha la Simba Day, huku ikiwapa jukumu la wasanii wanaoipenda klabu hiyo kuandaa kibao kitakachoisifia timu yao na kuchezwa katika mechi mbalimbali za timu hiyo.

**KUACHIA NGAZI**

Magori alisema kuwa anatarajia kuachia ngazi katika nafasi anayoishikilia baada ya siku 60 kumalizika.

Kiongozi huyo alisema kuwa uamuzi wa kuendelea kufanya kazi umetokana na Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo kumuomba, huku wakiahidi kuanza mchakato mpya wa kuajiri watendaji wengine.

"Mimi naona ninafaa zaidi kuwa kwenye bodi, niliombwa nisaidie kwa miezi sita, kuanzia Novemba (mwaka jana), katika kipindi hiki cha mpito, na kwa sasa nimekubali kwa sababu ni kipindi cha usajili na kuandaa timu, tutatangaza nafasi hii kwa ajili na nyingine hivi karibuni," Magori alisema.

## Amunike atabiri makubwa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, amesema kuwa anaamini kikosi chake kitafanya vema katika mechi za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) na hii inatokana na kuwajenga wachezaji wake kujiamini.

Amunike alisema hayo jana jioni kabla timu yake haijakutana na wenyeji Misri (Mafarao) katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa uliotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Borg El Gharab mjini Alexandria.

Mnigeria huyo aliyewahi kucheza katika timu ya Barcelona alisema kuwa wachezaji wake wamejifunza mambo mbalimbali kuelekea michuano hiyo na watakapomaliza watakuwa wameimarika.

Amunike alisema kwamba kukosa tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa miaka 39 si kigezo cha timu yake kutarajiwa kufanya vibaya, bali kiwango watakachokionyesha mwaka huu ndio kitatoa majibu halisi.

"Kuwa sehemu ya timu zinazoshiriki mashindano haya hapa Misri, ni nafasi kubwa, nina furaha kuona Tanzania imefanikiwa kupata nafasi hii, wachezaji wetu watapata fursa ya kujifunza zaidi, watakutana na wenzao wanaocheza ligi mbalimbali za Ulaya, watajifunza vitu ambavyo vitawaimarisha na kusaidia kunyanyua viwango vyao," alisema Amunike. Aliongeza kuwa amefurahia kupata mchezo dhidi ya Misri ambayo ina wachezaji wengi wazoefu na itamsaidia kufanya tathmini ya kikosi chake kilipofikia kabla ya kuanza kwa fainali hizo baadaye mwezi huu.

"Misri ni kipimo kizuri kwetu, itatusaidia kujua tufanye nini kabla ya kuelekea mechi yetu dhidi ya Senegal, najua kuna vitu tutajifunza kupitia mchezo huo," Amunike alisema.Naye Mkuu wa msafara wa timu hiyo ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Khalid Abdallah, alisema kuwa wachezaji wote 23 ambao wataiwakilisha nchi katika mashindano hayo wako salama na wanaendelea na programu za mazoezi kama ilivyopangwa.

"Wachezaji wako sawa, kila kitu kinakwenda vizuri, kilichobaki ni Watanzania mtuombee kwa Mungu ili malengo yetu yatimie, kwa faida ya nchi yetu," Abdallah alisema.

Stars iko Kundi C na itaanza mechi yake ya kwanza Juni 23 mwaka huu dhidi ya Senegal wakati siku ya ufunguzi, Misri wataikaribisha Zimbabwe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >